

# Mawazo Juu ya Maisha ya Roho



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 1

# Mawazo Juu ya
# Maisha ya Roho

Taasisi ya Ruhi

Vitabu vilivyopo katika Mfuatano:

Hapa chini kuna majina ya vitabu vya sasa vilivyopo katika mfuatano uliosanifiwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vimekusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika jitihada ya hatua kwa hatua ya kuongeza uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia inaendelea kukuza seti ya kozi ambazo zinachepuka kutoka kitabu cha tatu kilichopo katika mfuatano kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya Kibahá'í ya watoto, hali kadhalika seti nyingine kutoka Kitabu cha 5 kwa ajili ya kuwainua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hivi pia vimeainishwa katika orodha hapo chini. Sharti izingatiwe kwamba orodha hii inaweza kubadilika kadiri tajiriba ugani inavyoongezeka, na mada zaida zitaongezwa kadiri idadi ya vipengele vya mtaala vinavyoendelea kukuzwa vitakapofikia hatua ambapo vitaweza kupatikana kwa wingi.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinukaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa kwanza wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Duara Lipanukalo: Mchepuo wa pili wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Kufundisha Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja katika Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Agano la Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mjadala wa Umma* |

Hakimiliki © 1999, 2013, 2020 na Shirika la Ruhi, Kolombia
Haki zote zimehifadhiwa. 4.1.4.PE kilichapishwa Mei 2026
ISBN 978-958-52941-8-9

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Reflexiones sobre la vida del espíritu*
Hakimiliki © 1987, 1995, 2008, 2020 na Shirika la Ruhi, Kolombia
ISBN 978-958-59880-3-3

Taasisi ya Ruhi
Cali, Kolombia
Baruapepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo


Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi .................... v

Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í ................................ 1

Sala ...................................................................... 13

Uhai na Kifo .................................................................. 29

# Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi

Idadi ya maeneo ambapo *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho*, kitabu cha kwanza cha mlolongo mkuu wa kozi zinazotolewa na Taasisi ya Ruhi, kinachosomwa kote ulimwenguni yamekuwa yakiongezeka kwa miaka mingi. Katika hali nyingi, nyenzo husomwa na kujadiliwa na kikundi cha marafiki, ambao wanaweza kuunda kikundi cha mafunzo ambacho hukutana mara kwa mara, wanaweza kuja pamoja katika kampeni iliyoandaliwa kwa ajili ya ujifunzaji shadidi, au wanaweza kukusanyika katika kambi wakati wa likizo za shule. Nafasi yoyote iwayo, mshiriki mmoja wa kikundi huwa kama mkufunzi. Uhusiano kati ya mkufunzi na washiriki wengine siyo ule wa mwalimu na mwanafunzi; wote wanajihusisha kikamilifu katika mchakato ambamo kila mmoja anatafuta kujifunza. Lakini mkufunzi siyo mrahisishaji aliyejitenga na mtepetevu pia wa majadiliano. Baada ya kumaliza kusoma idadi ya kutosha ya kozi zilizomo katika mlolongo na kufanya vitendo vya huduma vinavyohamasishwa, anaweza kumsaidia kila mshiriki wa kikundi kutimiza kusudi la nyenzo inayosomwa. Wale wanaotenda kama wakufunzi wa Kitabu cha 1 wanaweza kuona inafaa kupitia upya mawazo yaliyowasilishwa katika utangulizi huu wakati hadi wakati.

Washiriki kote ulimwenguni huja kwenye kozi hii ya kwanza ya taasisi kutoka usuli tofauti. Baadhi tayari ni wana-jumuiya wa jumuiya ya Kibahá'í ambao wanatumaini kukuza uwezo wao wa kuhudumia Hoja waliyoikumbatia. Wengine huona kozi hii kama mwanzo wa uchunguzi wao wa Imani ya Kibahá'í kama dini. Bado wengine wanavutiwa na mawazo bora ya Kibahá'í na hupenda kujifahamisha wenyewe malengo na jitihada za jumuiya. Na kuna idadi iongezekayo ya vijana ambao hasa, wakitaka kukuza uwezo wao wa kuihudumia jamii, aghalabu kupitia programu moja au nyingine iliyoanzishwa na jumuiya ya Kibahá'í, wao huchukua kozi hiyo kama hatua ya awali.

Tangu mwanzoni inabidi iwe wazi kwa kila mshiriki kwamba kozi za Taasisi ya Ruhi zinachora njia ya huduma kwa jamii ya wanadamu, ambayo juu yake kila mmoja wetu hutembea kwa hatua yake, akiwasaidia na akisaidiwa na wengine. Kukanyaga njia hii humaanisha ufuatiliaji wa kusudi la kimaadili lenye pande mbili: kushughulika na ukuaji wa kiroho na kiakili wa mtu mwenyewe, na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Maendeleo kwenye njia hii hujumuisha ukuzaji wa idadi fulani ya uwezo ambao unahitaji uelewa na ujuzi, sifa za kiroho na mielekeo istahiliyo sifa, hali kadhalika wingi wa vipaji na stadi. Vyanzo vya maarifa ambavyo kutoka kwavyo vitabu vya Taasisi huchota kwa upande mmoja, ni mafundisho ya Imani ya Kibahá'í na, kwa upande mwingine, tajiriba inayokusanywa ya jumuiya ya Kibahá'í kote ulimwenguni katika kuendeleza ustaarabu wa kimwili na wa kiroho. Ni muono wa Bahá'u'lláh juu ya mtu binafsi anavyoweza kuwa na juu ya ustaarabu tunaoweza kuujenga ndivyo hutia msukumo Taasisi. Inadhaniwa kwamba washiriki wote, bila kujali usuli wao wapo huru kuukumbatia muono huu, ambao ni dhahiri katika kila kitengo cha kila kitabu.

Katika ulimwengu ambamo itikadi na falsafa zipo tayari kutumia kila njia iwezekanayo kwa ajili ya kupata wafuasi, mtu ambaye haijui vizuri Imani pengine anaweza kuwa na maswali halisi juu ya madhumuni ya Taasisi ya Ruhi, hususan, "Je, ninaombwa kubadili dini yangu?" au "Je, ninaombwa kujiunga na dini?" Maswali kama hayo humpa mkufunzi nafasi ya kuelezea kusudi la mlolongo wa kozi kama ilivyoelezwa kwa ufupi hapo juu. Wakati ni kawaida kwamba

Wabahá'í wangekuwa na shauku kuwaona marafiki zao wakijiunga na jumuiya, mafundisho yao wenyewe yanawazuia, dhidi ya kujishughulisha na kuwashawishi watu kubadili dini, mkufunzi angependa kuongezea. Kutembea Njia ya Huduma iliyoanzishwa na kozi za taasisi huhitaji uelewa uendeleao kuimarika wa Mafundisho ya Bahá'u'lláh, ambayo nyenzo hujitahidi kuyafafanua kwa uwazi; ridhaa na imani ni masuala yanayohitaji kutafakariwa na kila mtu kwa uhuru na bila shinikizo.

Haishangazi basi, ni pamoja na suala la uelewa, ambalo ni muhimu sana kwa vitabu vyote vya mlolongo, kwamba hiki huanza nalo. Kusoma Maandiko Matakatifu si sawa na kusoma maelfu ya kurasa ambazo mtu huziona maishani mwake, na kitengo, "Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í", hutaka kulea desturi ya kusoma vifungu kutoka Vitabu Vitakatifu kila siku na kutaamuli juu ya maana zake, desturi ambayo itawasaidia sana washiriki kadiri waanzavyo safari yao kwenye njia ya huduma. Ili kuwaongoza katika usomaji wake, mkufunzi sharti afikirie sana juu ya suala la uelewa.

Maandiko ya Kibahá'í yana kweli za kina za kiroho, na hata tunavyojitahidi kupiga hatua katika uelewa wetu wa maana zake zisizo na kikomo, tunajua kwamba kamwe hatuwezi kufikia mwisho kabisa. Kwa kawaida tunapata uelewa wa msingi wa maana ya papo hapo ya kifungu kimoja tunapokisoma kwa mara ya kwanza, na Sehemu ya 1 ya kitengo hiki hupachukulia hapo kama mahali pa kuanzia. Hivyo, baada ya kusoma nukuu hii, "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kwa matendo safi na mema, kwa mwenendo usifikao na unaostahili", washiriki wanaulizwa tu, "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwaje?" Kwa mtazamo wa haraka, sehemu kubwa ya maswali na mazoezi ya aina hii yanaonekana kuwa rahisi sana. Lakini miaka mingi ya tajiriba inaonekana kuthibitisha uamuzi wa Taasisi wa kuanza kwa namna hii. Sote tunahitaji kukumbushwa kwamba, katika haraka yake ya kutafuta matabaka ya ukweli katika kifungu kimoja, akili haipaswi kupuuzia maana yake dhahiri. Umakini kwa kiwango hiki cha kwanza cha uelewa pia unadhihirika kuwa muhimu kwa ushauriano wa kikundi; huimarisha umoja wa fikra, ambao hupatikana kwa urahisi pale ambapo maoni ya mtu binafsi yanaporuhusu kuangaziwa na hekima Takatifu.

Ni muhimu kuzingatia hapa kwamba uelewa wa maana ya papo hapo wa vifungu vingi zaidi hauna faida kutokana na majadiliano marefu juu ya neno moja moja nje ya muktadha. Baada ya kusema hayo, inaweza kuwa ya muhimu, wakati mwingine, kwa kikundi kuangalia neno katika kamusi. Kile ambacho kingefaa zaidi, hata hivyo, ni kwamba washiriki watajifunza jinsi ya kuelewa maana za maneno kutoka sentensi na aya nzima.

Ili uelewa uweze kupanuka zaidi ya milki ya maana ya papo hapo, mifano inayoonesha jinsi mawazo yanavyoweza kuelezwa kikamilifu inaweza kusaidia. Kile kinachohitajika kuhusiana na suala hili ni mazoezi ya moja kwa moja. Katika Sehemu ya 2, mathalani, washiriki wanaombwa kuamua, kufuatana na kifungu walichosoma hivi punde, ikiwa baadhi ya tabia zinastahili sifa. Katika zoezi kama hilo katika Sehemu ya 4, wanahamasishwa kutaja njema tano na kisha kuamua ikiwa inawezekana kupata hata mojawapo bila ukweli—kama ulivyoelezewa katika Maandiko kuwa ni "msingi wa njema zote za binadamu".

Ili kufanikisha kusudi lake, kitengo hiki kinahitaji kupiga hatua zaidi katika uelewa kwa kuwapa washiriki changamoto ya kufikiria juu ya baadhi ya matokeo ya vifungu vilivyowasilishwa. Katika Sehemu ya 2, wanatakiwa kuamua ikiwa kauli hii "Watu wema duniani ni wachache mno kwamba matendo yao hayana matokeo yoyote" ni kweli. Hapa nia siyo tu kutoa maoni. Mkufunzi lazima asite kidogo na kuhoji sababu ya majibu ya washiriki. Kwamba kauli hiyo siyo lazima iwe kweli kwa sababu inapingana na nukuu ya kwanza katika sehemu iliyotangulia ni hitimisho ambalo kikundi sharti kifikie. Swali kwamba ikiwa Wabahá'í

wanaweza kuungama dhambi zao kwa wengine pia ni mfano wa aina hii ya zoezi. Linaongelea katazo lililomo katika mafundisho dhidi ya kuungama kama njia ya ondoleo la dhambi, jambo ambalo ingawa halikutajwa wazi wazi katika vifungu vyovyote vilivyosomwa, linaweza kueleweka kwa kuchunguza maana ya aya hii, "Jifanyie hesabu mwenyewe kila siku kabla hujaitwa kutoa hesabu".

Kwa vyovyote mazoezi ya kitengo hiki hayajaribu kujumuisha uwanda mpana wa maana zilizomo katika vifungu vinavyozungumziwa. Suala moja ambalo kila mkufunzi lazima alifikirie ni muda kiasi gani mjadala unapaswa kuchukua katika zoezi lolote lile. Hapa ni muhimu kuzingatia kwamba kurefusha majadiliano kwa kutambulisha dhana nyingi zinazohusiana lakini zilizo nje hupunguza ufanisi wa nyenzo. Kila kikundi kinahitaji kuanzisha mdundo ufaao wa kusonga mbele, washiriki sharti waone dhahiri kwamba wanapiga hatua kwa uthabiti kulingana na uwezekano wao wenyewe. Mkufunzi, hata hivyo, lazima awe makini, isitokee kuwa sehemu zinapitiwa kwa haraka na kijuu-juu bila uchambuzi wa kina wa mazoezi; vikundi vilivyoendelea kwa njia hii, kwa kujaza tu majibu, kamwe havijafikia matokeo ya kudumu.

Jambo la mwisho linastahili kutajwa hapa: ni juu ya mkufunzi kuhakikisha kwamba kila mshiriki wa kikundi anaendelea kujihusisha na mchakato wa kujifunza unaoendelezwa na nyenzo. Kukaribisha ushiriki bila kumlazimisha mtu yeyote kuzungumza aghalabu ni changamoto. Kinachopaswa kufahamika tangu mwanzoni ni kwamba changamoto hii kwa nadra huondolewa kwa kuuliza maswali kama vile, "Hii humaanisha nini kwako?" Maswali ya aina hii hupunguza ufahamu na ukweli hadi kwenye kiwango cha maoni. Na hapo inathibitika kuwa vigumu kujenga mazingira ambamo ushauriano miongoni mwa washiriki wa kikundi hasa katika kuleta uelewa uongezekao.

Kitengo cha pili katika kitabu hiki kinahusu, kama kile cha kwanza desturi muhimu kwa maisha ya kiroho: kusali mara kwa mara. Katika sehemu ya ufunguzi kinaweka dhana ya "njia ya huduma", na kupendekeza kwamba, ili kutembea njia hii, lazima tuwe tumejawa na shauku ya kusudi lenye pande mbili. Washiriki wachunguze seti za awali za mateuzi zinazotoa umaizi katika asili ya kusudi hili, mada ambayo itazungumziwa zaidi katika kozi za siku za mbele.

Kwa kuzingatia mada hii, kitengo hiki kinaanza kuchunguza umuhimu wa sala. Kinatumia mbinu inayofanana na ile iliyoelezwa katika aya zilizotangulia. Maswali na mazoezi yanaundwa ili kuendeleza uelewa wa maana ya vifungu kutoka katika Maandiko yanayosomwa. Kadiri kikundi kinavyoendelea kupitia kitengo hiki, mkufunzi anaweza kuhitaji kuondoa mashaka kwa kuchambua dhana zilizojikita katika ufafanuzi na mazoea ya zamani. Katika baadhi ya tamaduni, kaida na maumbo ya nje pole pole yamefunika umuhimu wa hali ya ndani, na wengi sana hupuuzia hitaji la sala, ambayo, kwa roho ya mwanadamu, ni muhimu kama kilivyo chakula cha kustawisha mwili.

Zaidi ya yote, kwa hiyo, kitengo hiki kinatarajia kuamsha ndani ya washiriki shauku ya "kuzungumza na Mungu" na kuwa karibu Naye. Miongoni mwa mawazo yaliyozungumziwa ni humaanisha nini kuingia katika hali ya ibada, mwelekeo wa mioyo na akili tufanyapo hivyo, na hali zinazopaswa kujengwa katika mazingira yetu, tuwe peke yetu au katika mkusanyiko. Kwa hakika, baada ya kufikiria kidogo juu ya nguvu zinazozalishwa kupitia ibada ya pamoja, washiriki wanaombwa kufikiria kukaribisha mkusanyiko kwa ajili ya sala na ibada.

Usomaji wa kitengo cha tatu cha kitabu hiki, "Uhai na Kifo", inatarajiwa, utaimarisha azma ya Kutembea Njia ya Huduma na kuijalia maana ya ndani zaidi. Huduma katika

ulimwengu huu hueleweka vyema zaidi katika muktadha kamili wa maisha, ambayo huenda mbele zaidi ya maisha yetu ya hapa duniani na milele huendelea kadiri roho zetu zinavyoendelea katika malimwengu yote ya Mungu. Katika mchakato wa elimu, kinyume na mafunzo ya kiufundi, washiriki wanapaswa kuwa wenye utambuzi zaidi kuhusu maana na umuhimu wa kile wanachokifanya. Ni pale tu utambuzi huo utakapokua, tajiriba huonesha, ndipo watakapoweza kujiona kama "wahusika" amilifu wa ujifunzaji wao wenyewe.

Kila sehemu ya kitengo hiki huanza kwa nukuu moja hadi tatu kutoka Maandiko ya Kibahá'í, zikifuatiwa na mazoezi machache. Lugha ya vifungu vilivyonukuliwa katika kitengo hiki ni ngumu zaidi kuliko vile viwili vilivyotangulia. Hakuna haja bila shaka, kwa kikundi kujikita zaidi juu ya maneno magumu; mkufunzi atataka kuhakikisha kwamba kila mmoja anaelewa wazo kuu linalozungumziwa katika kila sehemu, jambo ambalo ndilo hasa mazoezi hujaribu kutoa.

Kwa kuzingatia asili ya somo, mazoezi yanayohusisha mifano halisi ni machache na hutokea kwa nadra. Sehemu kubwa huelekea kufanya kazi kwenye kiwango cha kinadharia. Kile kinachohitaji kukumbukwa ni kwamba baadhi ya maswali yanayoulizwa katika mazoezi haya hayawezi kujibiwa kwa haraka au kwa uwazi. Yanatambulishwa kwa ajili ya kukuza ufahamu wa somo hilo; kama washiriki hufikiria tu maswali kama haya, lengo la ujifunzaji litakuwa limetimizwa.

Sehemu kadhaa za mwanzoni zinalenga juu ya uhusiano kati ya roho na mwili, ambavyo kwa pamoja, humfanya mwanadamu katika ulimwengu huu wa uwepo. Wazo kuu linalowasilishwa katika sehemu hizi ni kwamba roho siyo kitu cha kimwili; uhusiano wake na mwili unaweza kulinganishwa na mwanga unaoonekana katika kioo. Si vumbi lifunikalo uso wake wala uharibifu wa kioo hatimaye viwezavyo kuathiri mng'ao wa mwanga wenyewe. Kifo ni badiliko tu la hali, pale uhusiano kati ya mwili na roho unapovunjika; hatimaye, roho huendelea milele kuelekea kwa Muumba wake.

Kitengo hiki hugeukia tena kwenye suala la kusudi la maisha—kumjua Mungu na kufika Mbele Yake. Majadiliano hapa yanazungukia mada mbili pana. Ya kwanza ni kusudi la maisha yetu katika ulimwengu huu na ya pili ni safari ya roho baada ya kifo. Roho ni ishara ya Mungu na inaweza kuakisi majina na sifa Zake zote. Hata hivyo uwezo uliomo ndani ya mwanadamu umejificha, unaweza kukuzwa tu kwa msaada wa Wadhihirishaji wa Mungu, wale Viumbe waliotakasika Ambao huja wakati hadi wakati kuwaongoza wanadamu. Kupitia elimu ya kiroho Wanayoleta, hazina zilizofichwa ndani mwetu zinaweza kufunuliwa.

Kuhusu safari ya roho baada ya kifo, mfuatano wa mawazo umewekwa wazi kwa ajili ya washiriki kutafakari: kwamba wale walio waminifu kwa Mungu watafikia kwenye furaha ya kweli; kwa kuwa hakuna yeyote kati yetu anayeweza kujua mwisho wake mwenyewe, na kwa hiyo inatubidi tusameheane, na tusjihisi bora kuliko wengine; kwamba katika ulimwengu ujao, kama ilivyo katika ulimwengu huu, roho itaendelea kwenda mbele na vipawa vya kiroho tulivyovikuza hapa vitatuauni na kutatusaidia huko, kwamba tutawatambua wapendwa wetu katika milki za mbali zaidi, tutakumbuka maisha yetu katika ulimwengu huu, na tutafurahia urafiki na roho takatifu na zilizotakasika.

Kitengo kinahitimishwa kwa kifungu kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh ambamo tunahakikishiwa manufaa ya ulimwengu ujao na kuhimizwa kwamba tusiruhusu mabadiliko na nasibu za maisha haya kutuletea huzuni. Washiriki wanaombwa kutafakari, kisha, juu ya maana za yale waliyojifunza kwa ajili ya maisha yao wenyewe.



# Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í

## Kusudi

Kuimarisha desturi ya kusoma vifungu kutoka Maandiko Matakatifu kila siku na kutafakari juu ya maana zake

## SEHEMU YA 1

Kusudi la kitengo hiki ni kukusaidia kujenga na kuimarisha desturi ya kusoma vifungu kutoka Maandiko Matakatifu kila siku na kutafakari juu ya maana zake. Kitengo kinaanza kwa zoezi rahisi linalokutaka kusoma kauli ya sentensi moja kutoka Maandiko na kujibu swali, ambapo jibu lake ni kauli yenyewe. Ingawa ni rahisi kulifanya, zoezi hili litakusaidia kutafakari juu ya maana ya kauli zilizotajwa na kuzikariri.

**"Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kwa matendo safi na mema, kwa mwenendo usifikao na unaostahili."[1]**

1. Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwaje? ______________________________

_____________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________________

**"Jihadharini, Enyi watu wa Bahá, msije mkatembea katika njia za wale ambao maneno yao hutofautiana na matendo yao."[2]**

2. Je, ni katika njia za watu gani tusitembee? ____________________________________

_____________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________________

**"Ewe Mwana wa Kuwa! Jifanyie hesabu mwenyewe kila siku kabla hujaitwa kutoa hesabu …"[3]**

3. Je, yatupasa kufanya nini kabla hatujaitwa kutoa hesabu? _______________________

_____________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________________

**"Sema: Enyi ndugu! Acheni matendo, siyo maneno, yawe pambo lenu."[4]**

4. Pambo letu la kweli linapaswa kuwa lipi? _______________________________________

_____________________________________________________________________________

**"Maneno matakatifu na matendo safi na mema hupaa hadi mbingu ya utukufu wa mbinguni."[5]**

5. Je, maneno matakatifu na matendo safi na mema hufanya nini? __________________

_____________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 2

Hapa chini kuna mazoezi kadhaa yanayohusiana na nukuu ambazo ndiyo tu mmezisoma. Yamekusudiwa kukusaidia kutafakari zaidi juu ya maana ya vifungu katika kikundi chenu na yasifanywe bila kufikiri. Hii haimaanishi kwamba kila zoezi linahitaji majadiliano marefu. Kama swali lina changamoto, hata hivyo, mkufunzi wa kikundi chenu atawakusaidia kulichunguza kikamilifu.

1. Ikiwa jambo ni la “kusifika” humaanisha kitu kinachostahili sifa. Ni yapi kati ya yafuatayo yanastahili sifa?

    _____ Kuwa mfanyakazi mzuri

    _____ Kuheshimu wengine

    _____ Kuwa mwenye bidii katika masomo

    _____ Kuwa mwongo

    _____ Kuwa mvivu

    _____ Kuwahudumia wengine

2. Je, kirai “kabla hujaitwa kutoa hesabu” humaanisha nini? ______________________

    ________________________________________________________________________

3. Ni zipi kati ya kauli zifuatazo ni za kweli?

    _____ Kuna watu wema wachache mno duniani kwamba matendo yao hayana matokeo yoyote.

    _____ Jambo fulani ni sahihi likikubaliana na maoni ya watu wengine.

    _____ Jambo fulani ni sahihi likikubaliana na Mafundisho ya Mungu.

4. Ni yapi kati ya yafuatayo ni matendo safi na mema?

    _____ Kuwatunza na kuwafundisha watoto

    _____ Kuiba

    _____ Kusali kwa ajili ya maendeleo ya wengine

    _____ Kusema uwongo kidogo ili kuepuka taabu

    _____ Kuwasaidia wengine na kutarajia zawadi

5. Ni katika hali zipi miongoni mwa zifuatazo maneno ya mtu hutofautiana na matendo yake?

    _____ Mtu huendelea kurudia rudia kwamba wote tunapaswa tuwe wamoja lakini hutenda kwa namna inayotengeneza mgogoro.

    _____ Mtu husifu thamani ya maisha ya ubikira lakini ana uhusiano wa ngono nje ya ndoa.

_____ Mtu anakunywa pombe mara moja moja wakati huo huo anadai kufuata imani ya kidini inayokataza unywaji wa pombe.

_____ Mtu anatetea usawa wa wanaume na wanawake, lakini, akiwa kama mwajiri huwalipa wanawake ujira kidogo kuliko wanaume kwa kazi hiyo hiyo.

6. Je, inaruhusiwa kwa Mbahá'í kuungama kwa mtu mwingine? ___________________

7. Je, inampasa afanye nini badala ya kuungama? ________________________________
________________________________________________________________________

8. Je, kirai "mbingu ya utukufu wa mbinguni" humaanisha nini? ___________________
________________________________________________________________________

9. Je, matendo maovu yana matokeo gani duniani? _______________________________
________________________________________________________________________

10. Je, matendo maovu yana matokeo gani wale wanaoyatenda? ____________________
________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 3

Sasa soma na tafakari juu ya nukuu zifuatazo kutoka Maandiko, kisha jaribu kuzikariri.

**"Ukweli ndiyo msingi wa njema zote za binadamu."**[6]

1. Ni upi msingi wa njema zote za binadamu? ____________________________________
________________________________________________________________________

**"Bila ukweli maendeleo na mafanikio, katika malimwengu yote ya Mungu, hayawezekani kwa roho yoyote ile."**[7]

2. Ni nini kisichowezekana bila ukweli? ________________________________________
________________________________________________________________________

**"Rembesheni ndimi zetu, Enyi watu, kwa ukweli, na pambeni roho zenu kwa pambo la uaminifu."**[8]

3. Ni kwa kitu gani turembeshe ndimi zetu? _____________________________________
________________________________________________________________________

4. Ni kwa kitu gani tupambe roho zetu?________________________________________

________________________________________________________________________

**"Acha jicho lako liwe safi, mkono wako mwaminifu, ulimi wako wa ukweli, na moyo wako mwongofu."[9]**

5. Jicho letu linapaswa liweje? ________________ Mkono wetu? _________________

Ulimi wetu? _______________________ Moyo wetu?________________________

**"Wale wanaoishi ndani ya Hekalu Takatifu la Mungu, na kusimikwa kwenye viti vya utukufu wa milele, watakataa, hata kama wakiwa wanakufa kwa njaa, kunyoosha mikono yao, na kunyang'anya kinyume cha sheria mali ya jirani yao, japokuwa awe muovu na asiye na thamani."[10]**

6. Tunapaswa tufanye nini hata kama tunakufa kwa njaa? _______________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Kama pengine mlivyoona katika Sehemu ya 2, baadhi ya mazoezi katika kitengo hiki yanahitaji majibu kamili. Katika hali kama hizo, kama kuna wasiwasi kuhusu jibu, mkufunzi wa kikundi chako ataweza kukusaidia wewe na washiriki wenzako kufikia umoja wa fikra. Kwa mazoezi mengine, ni maongezi yenyewe ambayo yana thamani, na siyo jibu moja maalum linalotarajiwa. Katika mazoezi yafuatayo, zoezi la 3 ni la aina ya kwanza, wakati zoezi la 6 hudondokea kwenye aina ya pili.

1. Ukweli ndiyo msingi wa njema zote za binadamu. Orodhesha njema tano: ________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

2. Je, tunaweza kujipatia njema hizi bila ukweli? ______________________________

3. Zipi kati ya kauli zifuatazo ni kweli?

_____ Mtu anaweza kuwa mwenye haki hata kama anasema uwongo.

_____ Mtu anayeiba ana mkono mwaminifu.

_____ Mkono mwaminifu kamwe haugusa kile kisicho chake.

_____ Kuangalia nyenzo za ponografia ni kinyume na ushauri wa Bahá'u'lláh wa kuwa na jicho lililo safi.

_____ Ukweli humaanisha kutodanganya.

______ Uaminifu ni pambo la roho.

______ Mtu ambaye si mkweli anaweza kuendelea kiroho.

______ Ni sawa kusema uwongo mara moja moja.

______ Kuiba kunakubaliwa mbele ya Mungu ikiwa mtu ana njaa.

______ Kuchukua kitu bila ruhusa ya mwenyewe, tukifikiri kwamba tutakirudisha baadaye, siyo kuiba.

______ Tukitenda kwa uaminifu na kuwa wenye haki na wakweli, moyo wetu ni mwongofu.

______ Haiwezekani kuifanya biashara ifanikiwe bila kudanganya kidogo.

4. Je, inawezekana mtu kujidanganya mwenyewe? ____________________________

5. Kitu gani tunachopoteza tunaposema uwongo? ____________________________

6. Dunia ingekuwaje kama sote tungekuwa wenye ukweli na waaminifu? ____________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Soma nukuu zifuatazo na jaribu kujifunza kimoyomoyo. Kukariri nukuu kutoka katika Maandiko ni jambo lenye faida sana, na inabidi ujitahidi sana kufanya hivyo. Si kila mtu, bila shaka, anaweza kukariri vifungu kiurahisi. Walakini, kufanya juhudi hutusaidia kuweka mawazo mioyoni na akilini mwetu na kuvisema kwa maneno yaliyo karibu na maandiko chanzi kadiri iwezekanavyo.

> **“Ulimi mwema ni sumaku ya mioyo ya watu. Ni mkate wa roho, unavika maneno kwa maana. Ni chemchemi ya mwangaza wa hekima na ufahamu.”**[11]

1. Ulimi mwema unaweza kuelezwaje? ____________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________

2. Ni matokeo gani ulimi mwema unayo juu ya maneno? ______________________
________________________________________________________________

**"Enyi wapendwa wa Bwana! Katika Kipindi hiki kikuu Kitakatifu, ugomvi na ushindani kwa vyovyote haviruhusiwi kamwe. Kila mshari hujinyima mwenyewe neema za Mungu."[12]**

3. Kulingana na ya hapo juu, nini hakiruhusiwi Kipindi hiki Kitakatifu? ____________
________________________________________________________________________

4. Mshari hujifanyima nini mwenyewe? ______________________________________
________________________________________________________________________

**"Hakuna chochote kinachoweza, katika Siku hii, kutia madhara makubwa zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na mabishano, utengano na utepetevu, miongoni mwa wapendwa wa Mungu."[13]**

5. Ni hali zipi zinaweza kutia madhara makubwa mno kwenye hoja ya Mungu? ______
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

**"Usiridhike na kuonesha urafiki kwa maneno tu; acha moyo wako uwake kwa wema wa upendo kwa wale wote ambao waweza kupita njia yako."[14]**

6. Ni aina gani ya urafiki ambayo haipaswi kuturidhisha?________________________
________________________________________________________________________

7. Ni nini kinapaswa kuwaka kwa wangavu katika moyo wetu? ___________________
________________________________________________________________________

**"Wakati wazo la vita likija lipinge kwa wazo la nguvu zaidi la amani. Wazo la chuki lazima liangamizwe kwa wazo la uwezo zaidi la upendo."[15]**

8. Ni kwa kitu gani wazo la vita linapaswa lipingwe? ___________________________
________________________________________________________________________

9. Ni kwa kitu gani wazo la chuki linapazwa liangamizwe? ______________________
________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Ukiwa na nukuu za hapo juu akilini, fanya mazoezi yafuatayo:

1. “Sumaku” ni neno lingine la kuelezea kitu kinachovuta kitu kingine. Ni kwa namna gani ulimi mwema unaweza kutenda kama sumaku? ____________________________

______________________________________________________________________________

2. Ni zipi kati ya kauli zifuatazo hutoka kwenye ulimi mwema?

_____ “Usinisumbue!”

_____ “Kwa nini huelewi hili?”

_____ “Tafadhali, ungependa kusubiri?”

_____ “Watoto wabaya jinsi gani!”

_____ “Shukrani, wewe ni mwema sana.”

_____ “Sina muda wowote kwa ajili yako sasa. Nina kazi nyingi?”

3. Ni zipi kati ya hali zifuatazo huonesha ugomvi na ushindani?

_____ Watu wawili hutoa mawazo tofauti juu ya mada fulani wakati wa ushauriano.

_____ Watu wawili wanakasirikiana na kubishana wakati wa ushauriano.

_____ Watu wawili wanaacha kuhudhuria mkutano wa ibada wa kila juma kwa sababu hawaelewani.

_____ Wajumbe wa timu inayoshirikiana katika mradi fulani wanaendelea kulalamika, kila mmoja anasema kwamba wengine hawatimizi wajibu wao.

4. Zipi kati ya hali zifuatazo huonesha dalili za utengano?

_____ Marafiki wawili wanapishana mtaani lakini wanapuuziana.

_____ Mtu mmoja anafika kwenye mkusanyiko wa ibada, na kila mmoja anamsalimia kwa furaha.

_____ Ingawa wanaheshimiana, wajumbe wawili wa kikundi hawataki kushiriki kwa pamoja katika mradi.

5. Amua ikiwa kauli zifuatazo ni za kweli:

_____ Mtu anapaswa aseme kwa uhalisi yale anayofikiria kuhusu wengine na haidhuru kama mioyo yao itachukizwa.

_____ Ni sawa kusema uwongo ili kujiepusha na ugomvi.

_____ Ugomvi unaweza kushindwa kwa upendo na wema.

_____ Maneno yana matokeo zaidi yakisemwa kwa upendo.

_____ Ni sawa kupigana na mtu mwingine kama akianza.

_____ Mtu ana haki ya kuwa mkali kwa wengine anapokuwa mgonjwa au na huzuni.

_____ Si jambo jema kuwacheka wengine wakoseapo.

_____ Kunapokuwepo na hisia kali kati ya marafiki, kila mmoja yafaa afanye jitihada maalum kumkaribia mwingine.

_____ Kunapokuwepo na hisia kali kati ya marafiki, kila mmoja yafaa asubiri hadi mwingine afanye jitihada kumkaribia.

## SEHEMU YA 7

Soma nukuu za hapo chini na uzikariri:

**"… Usengenyaji huzima mwanga wa moyo, na hufisha uhai wa roho."**[16]

**"Usinong'one dhambi za wengine iwapo wewe mwenyewe ni mtenda dhambi."**[17]

**"Usiseme uovu, ili usiweze kuusikia ukisemwa kwako, na usiyakuze makosa ya wengine ili makosa yako mwenyewe yasije yakaonekana makubwa …"**[18]

**"Ewe Mwana wa Kuwa! Ungewezaje kuyasahau makosa yako mwenyewe na kujishughulisha na makosa ya wengine?"**[19]

1. Usengenyaji una matokeo gani kwa yule anayesengenya? ______________________

______________________________________________________________________

2. Yatupasa tufikirie nini kabla ya kunong'ona dhambi za wengine? ______________

______________________________________________________________________

3. Nini kitatokea kwetu kama tukiyakuza makosa ya wengine? ___________________

______________________________________________________________________

4. Nini yatupasa tukumbuke tunapofikiria juu ya makosa ya watu wengine? ________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 8

Ukiwa na nukuu za hapo juu akilini, fanya mazoezi yafuatayo:

1. Nini hutokea kwa maendeleo ya roho ya mtu ambaye kujishughulisha na makosa ya watu wengine? ______________________________________________________

2. Je, usengenyaji una matokeo gani kwa jumuiya?______________________________

______________________________________________________________________

3. Utafanya nini wakati rafiki mmoja anaanza kuzungumza juu ya makosa ya mtu mwingine? ___________________________________________________________

___________________________________________________________________

4. Amua ikiwa kauli zifuatazo ni za kweli:

_____ Tunapozungumzia juu ya makosa halisi ya mtu hatusengenyi.

_____ Tunapozungumzia juu ya sifa nzuri za mtu na makosa yake wakati huo huo hatusengenyi.

_____ Usengenyaji umekuwa desturi katika jamii yetu na yatupasa kujenga nidhamu ya kuepukana nao.

_____ Msikilizaji akiahidi kutorudia yale tunayoyasema juu ya mtu mwingine, hakuna madhara katika usengenyaji.

_____ Usengenyaji ni moja ya maadui wakubwa kabisa wa umoja.

_____ Tukijipatia mazoea ya kuzungumza juu ya watu wengine wakati wote, tunaweza kuangukia katika usengenyaji kwa urahisi.

_____ Wakati uwezo wa watu mbalimbali unapojadiliwa katika mkutano wa Baraza la Kiroho la Mahali ili kuteua wajumbe wa kamati, huu ni usengenyaji.

_____ Tunapohisi msukumo wa kusengenya, yatupasa tuyakumbuke makosa yetu wenyewe.

_____ Tukijua mtu fulani anafanya jambo ambalo linaidhuru Imani, tunapaswa tulijadili na wana-jumuiya.

_____ Tukijua mtu fulani anafanya jambo ambalo linaidhuru Imani, tunapaswa tulitaarifu tu Baraza la Kiroho la Mahali.

_____ Siyo kosa kwa wanandoa kuzungumza juu ya makosa ya wengine kwani hawapaswi kutunza siri kati yao.

## SEHEMU YA 9

Kusudi la kitengo hiki, kama ilivyotajwa hapo mwanzoni ni kuwasaidia washiriki katika juhudi zao za kujenga na kuimarisha desturi ya kusoma vifungu kutoka Maandiko Matakatifu kila siku na kutafakari juu ya maana zake. Kusoma aya za Mungu kila asubuhi na jioni ni fundisho la Bahá'u'lláh linalochangia ukuaji wetu wa kiroho. Kifungu kifuatacho kinatukumbusha kuhusu fadhili tunazopata kwa kutimiza wajibu huu na unahamasishwa kukikariri:

> **"Jizamisheni wenyewe katika bahari ya maneno Yangu, ili muweze kufumbua siri zake na kugundua lulu zote za hekima ambazo zimefichika katika vina vyake."[20]**

Baada ya kumaliza kitengo hiki, pengine sasa ungependa kupata kitabu cha maandiko ya Bahá'u'lláh na kukisoma kila siku. Maneno Yaliyofichwa ni chaguo zuri la kwanza.

# MAREJELEO


1. Bahá’u’lláh, ikitajwa na Shoghi Effendi, katika *The Advent of Divine Justice* [Majilio ya Haki Takatifu] (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, chapisho la 2018), aya. 39, ku. 36–37. (toleo la Kiingereza)

2. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, chapisho la 2017), CXXXIX, aya. 8, uk. 345. (toleo la Kiingereza)

3. Bahá’u’lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá’í wa Tanzania, chapisho la 2017), Kiarabu na. 31, uk. 9.

4. Kama hapo juu, Kiajemi na. 5, uk. 22.

5. Kama hapo juu, Kiajemi na. 69, uk. 45.

6. ‘Abdu’l-Bahá, ikitajwa na Shoghi Effendi, katika *The Advent of Divine Justice* [Majilio ya Haki Takatifu], aya. 40, uk. 39.

7. Kama hapo juu.

8. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXXXVI, aya. 6, uk. 336.

9. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, chapisho la 2005), na. 9.5, uk. 138. (toleo la Kiingereza)

10. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXXXVII, aya. 3, uk. 338.

11. Kama hapo juu, CXXXII, aya. 5, uk. 327.

12. *Will and Testament of ‘Abdu’l-Bahá* [Wasia na Agano la ‘Abdu’l-Bahá] (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1944, chapisho la 2013), uk. 26. (toleo la Kiingereza)

13. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, V, aya. 5, uk. 8.

14. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa 16 na 17 Oktoba 1911, yaliyochapishwa katika *Hekima ya ‘Abdu’l-Bahá (Mazungumzo ya Paris): Hotuba Zilizotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, chapisho la 2016), na. 1.7, uk. 6. (toleo la Kiingereza)

15. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa na Abdu’l-Bahá 21 Oktoba 1911, kama hapo juu, na. 6.7, uk. 22.

16. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXXV, aya. 3, uk. 300.

17. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiarabu na. 27, uk. 8.

18. Kama hapo juu, Kiajemi na. 44, uk. 36.

19. Kama hapo juu, Kiarabu na. 26, uk. 8.

20. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, LXX, aya. 2, uk. 154.



# Sala

## Kusudi

Kutafakari juu ya umuhimu wa sala na kuimarisha desturi ya kusali mara kwa mara

## SEHEMU YA 1

Kozi za Taasisi ya Ruhi zimekusudiwa kuwasaidia washiriki kutembea njia ya huduma. Tunatembea njia hii tukisukumwa na hisia ya kusudi lenye pande mbili—kukua kiroho na kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Vipengele hivi viwili vya kusudi letu havitenganishiki. Bahá'u'lláh hutusihi katika kifungu kimoja:

> **"Msijishughulishe na mambo yenu wenyewe; acheni mawazo yenu yakaziwe juu ya kile ambacho kurejesha hali ya wanadamu na kutakasa mioyo na roho za watu."[1]**

Katika kifungu kingine, Yeye huweka wazi:

> **"… kusudi ambalo kwalo watu wa umauti, kutoka utupu kamili, wameingia katika milki ya uwepo, ni ili waweze kufanya kazi kwa ajili ya hali bora ya ulimwengu na kuishi pamoja kwa uelewano na upatano."[2]**

Kuhusiana na hali yetu ya ndani, Yeye hutamka:

> **"Moyo safi ni kama kioo; usafishe kwa mng'ao wa upendo na kujitenga na vyote isipokuwa Mungu, ili jua la kweli liweze kung'aa ndani mwake na alfajiri ya milele ipambazuke."[3]**

Na 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Mioyo yenu sharti iwe safi na dhamira zenu za dhati ili muweze kuwa wapokeaji wa majaliwa matakatifu."[4]**

1. Mawazo na shughuli zetu zinapaswa zielekezwe kwenye nini? __________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Kwa kusudi gani tumetoka kwenye utupu kamili na kuingia katika milki ya uwepo?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Ni kwa kitu gani tunapaswa kusafisha kioo cha moyo wetu? ____________________

______________________________________________________________________

4. Ni zipi baadhi ya hali zinazovutia majaliwa matakatifu?________________________

______________________________________________________________________

5. Je, kuna ukweli wowote kati ya yafuatayo?

   – Kwanza inabidi ujitunze mwenyewe, ndipo uwatunze wengine.

- Kama daima unawasaidia wengine, utaishia kupoteza malengo yako.
- Wewe mwenyewe ndiye rafiki yako wa karibu zaidi.
- Jambo muhimu ni kugundua kile kinachokufurahisha.
- Fuata ndoto zako, nazo zitakupeleka kwenye furaha.
- Maadam tu humuumizi mtu mwingine yeyote, haiidhuru nini unafanya.
- Ni sawa tu kuwa na nia za kibinafsi, maadam unafanya wema fulani.

## SEHEMU YA 2

Imani kubwa kwa kusudi letu lenye pande mbili ni kwamba sote tumeumbwa bora. Bahá'u'lláh husema:

> **"Ewe Mwana wa Roho! Nilikuumba tajiri; kwa nini unajishusha kwenye ufukara? Nilikuumba bora, kwa nini unajishusha? Kutoka katika kiini cha maarifa Nilikupa uhai, kwa nini unatafuta elimu kutoka kwa mwingine kando Yangu? Kutoka katika udongo wa upendo Nilikuumba, kwa jinsi gani unajishughulisha na mwingine? Geuzia macho yako kwako mwenyewe, ili uweze kuniona nikisimama ndani mwako mwenye nguvu, mwenye uwezo na ajitoshelezaye."**[5]

Kwa kujaza nafasi zilizo wazi hapa chini itakusaidia kutafakari juu ya kifungu hiki.

"Ewe Mwana wa Roho! Nilikuumba __________ ; kwa nini unajishusha kwenye ____________ ? ______________________ , kwa nini ________________ ? Kutoka katika __________ cha _____________ Nilikupa uhai, kwa nini _________________ _________ kutoka kwa mwingine kando _________________ ? Kutoka katika udongo wa ___________________________ , kwa jinsi gani __________________________ na _________________ ? Geuzia ____________ yako __________ mwenyewe, ili uweze kuniona nikisimama ndani mwako _______________________ , ___________ ____________ na ______________________ ."

Kuwa wakweli kwa ubora wa roho zetu, lazima tugeukie kwenye Chanzo cha uwepo wetu na kutafuta wongofu kutoka Kwake. Ili kufanikisha hili mojawapo ya njia za uhakika ni kupitia sala. Shoghi Effendi, Mlinzi wa Imani, hutuambia kwamba lengo lake kuu ni "maendeleo ya mtu binafsi na jamii, kupitia upataji wa njema za kiroho na vipaswa. Ni roho ya mtu ambayo sharti ilishwe kwanza. Na chakula hiki cha kiroho sala inaweza kukitoa vizuri zaidi."[6]

## SEHEMU YA 3

Mungu yu Mjua-Vyote, Mwenye Hekima-Kabisa. Yeye alituumba na anajua kile kilichomo mioyoni mwetu na kile kilicho bora kabisa kwa ajili yetu. Yeye hahitaji sala zetu. Sasa kwa nini tunasali?

'Abdu'l-Bahá husema:

**"Katika sala ya hali ya juu kabisa, watu husali tu kwa ajili ya upendo wa Mungu, siyo kwa sababu wanamuogopa Yeye au jahanam, au hutumaini kupata fadhili au pepo.… Pale mtu ampendapo mwanadamu mwingine, hawezi kujizuia kutaja jina la mpenzi wake. Ni vigumu jinsi gani kuendelea kutotaja Jina la Mungu wakati mtu amekwishampenda Yeye.… Mtu wa kiroho hapati furaha katika chochote kile ila katika kumbukumbu ya Mungu."**[7]

Na, katika kujibu swali moja, Yeye hueleza:

**"Ikiwa rafiki mmoja humpenda mwingine, si ni kawaida kwamba angependa kuseme hivyo? Hata kama anajua kwamba rafiki huyo anafahamu upendo wake, si bado angependa kumwambia juu ya jambo hilo?… Ni kweli kwamba Mungu anajua matakwa ya mioyo yote; lakini msukumo wa kusasli ni ule wa kawaida, ukibubujika kutoka upendo wa mtu kwa Mungu."**[8]

1. Kamilisha sentensi zifuatazos:

   a. Katika sala ya________________ , tuna ________ tu kwa ajili ya _______ wa Mungu, siyo kwa sababu tunamuogopa Yeye au ___________ , au hutumaini kupata ____________ au ____________ .

   b. Pale _____________ mwanadamu mwingine, ni __________________ kwetu kuendelea kutotaja __________ la ____________ wetu. ______________ jinsi gani kuendelea ___________ Jina la__________ wakati mtu _____________ Yeye.

   c. Mtu wa kiroho hapati _____________ katika chochote ila katika ______________ ____________ ya Mungu.

2. Kwa nini tunasali? _____________________________________________________

   _____________________________________________________________________

3. Kirai "kumbukumbu ya Mungu" humaanisha nini? ___________________________

   _____________________________________________________________________

4. Ni yapi matanaio ya hali ya juu kabisa ya mtu ambaye humpenda mwingine? _____

   _____________________________________________________________________

5. Msukumo wa kusali unabubujika kutokea wapi?______________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Katika sala iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh, tunasoma:

**"Nakusihi Wewe … kuifanya sala yangu moto ambao utateketeza tando ambazo zimenifungia nje kutoka uzuri Wako, na mwanga ambao utaniongoza kwenye bahari ya Uwepo Wako."[9]**

Katika sala hiyo hiyo tunamuomba Mungu:

**"Ifanye sala yangu, Ee Bwana Wangu, chemchemi ya maji ya uzima ambayo kwayo niweze kuishi kadiri enzi Yako idumuvyo, na niweze kukutaja Wewe katika kila ulimwengu wa malimwengu Yako."[10]**

1. Ni katika mantiki gani sala inaweza kuwa kama moto? Inateketeza nini?__________

________________________________________________________________________

2. Taja baadhi ya tando zinazotufungia nje kutoka kwa Mungu:____________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

3. Je, sala inaweza kuwa kama mwanga? Inatuongoza kuelekea wapi? ______________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

4. Je, sala inaweza kuwa kama chemchemi ya maji ya uzima? Inajalia nini kwenye roho zetu? ____________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Soma na utafakari juu ya maneno yafuatayo ya 'Abdu'l-Bahá:

**"Hakuna kitu kitamu zaidi katika ulimwengu wa uhai kuliko sala. Binadamu lazima aishi katika hali ya sala. Hali iliyobarikiwa kabisa ni hali ya sala na maombi. Sala ni mazungumzo na Mungu. Kufikia ukamilifu wa juu kabisa au hali iliyotamu zaidi si vinginevyo ila mazungumzo na Mungu. Hufanyiza hali ya**

**kiroho, hufanyiza ufahamivu na hisia za mbinguni, husababisha mivuto mipya ya Ufalme na husababisha wepesi wa kuhisi wa akili ya juu zaidi.”**[11]

1. Ni hali gani iliyo tamu zaidi katika ulimwengu wa uhai? ______________________

______________________________________________________________

2. Kirai “hali ya sala” humaanisha nini? ______________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

3. Taja baadhi ya sifa zinazoletwa na sala: ____________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

4. Pitia nukuu ambazo mmekwishasoma katika sehemu hizi chache na andika sentensi tano juu ya asili ya sala.

   - Sala ni ______________________________________________
   - Sala ni ______________________________________________
   - Sala ni ______________________________________________
   - Sala ni ______________________________________________
   - Sala ni ______________________________________________

## SEHEMU YA 6

Soma maneno yafuatayo ya Bahá’u’lláh na yatafakari:

**“Imba, Ee mtumishi Wangu, aya za Mungu ambazo umezipokea, kama ziimbwavyo na wale ambao wamemkaribia Yeye, ili utamu wa wimbo wako mzuri uweze kuiwasha roho yako mwenyewe, na kuvutia mioyo ya watu wote. Yeyote aghaniye, faraghani chumbani mwake, aya hizi zilizofunuliwa na Mungu, malaika watawanyao wa Mwenyezi watatawanyia mbali manukato ya maneno yatamkwayo na kinywa chake, na yatasababisha kila moyo wa mtu mwadilifu kupuma. Ingawa, mwanzoni anaweza kubaki bila kujua matokeo yake, lakini uwezo wa neema ijaliwayo kwake lazima, papo hapo au baadaye, ulete athari zake katika roho yake, hivyo ndivyo siri za Ufunuo wa Mungu zilivyoamriwa kwa uwezo wa Mapenzi ya Yeye Ambaye ni chanzo cha uwezo na hekima.”**[12]

1. Je, neno “imba” humaanisha nini? ________________________________

______________________________________________________________

2. Jinsi gani tunapaswa kuziimba aya za Mungu? ______________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Je, neno "sema" humaanisha nini? ______________________________

______________________________________________________________________

4. Je, neno "tawanya" humaanisha nini? ______________________________

______________________________________________________________________

5. Ni athari gani utamu wa wimbo wetu utakuwa nazo kwenye roho zetu? __________

______________________________________________________________________

6. Ni athari gani utamu wa wimbo wetu utakuwa nazo kwenye mioyo ya wengine? ___

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Pengine ungependa kukariri vifungu viwili kutoka sala iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh:

**"Ee Mungu, Mungu wangu! Usiangalie matumaini yangu na matendo yangu, la, afadhali zaidi uangalie mapenzi Yako ambayo yamezunguka mbingu na dunia. Kwa Jina Lako Kuu Kabisa, Ewe Bwana wa mataifa yote! Nimekitamani tu kile Wewe ulichokitamani, na kupenda tu kile Wewe ukipendacho."[13]**

**"Wewe u juu mno kwa sifa ya wale ambao wapo karibu Nawe kupaa kwenye mbingu ya ukaribu Wako, au kwa ndege wa mioyo ya wale ambao wamejitoa kwako kufikia mlango wa lango Lako. Ninashuhudia kwamba Wewe umetakasika kupita sifa zote na mtakatifu kupita majina yote. Hakuna Mungu ila Wewe, Aliyetukuka kuliko wote, Mtukufu-Kabis."[14]**

## SEHEMU YA 8

'Abdu'l-Bahá husema:

**"Inambidi mtumishi asali na atafute usaidizi kutoka kwa Mungu, na kuomba na kusihi msaada Wake. Hilo ndilo linalostahili daraja la utumishi, na Bwana ataamuru chochote Apendacho, kufuatana na hekima Yake kamili."[15]**

Na Yeye hueleza:

> **“Roho ina mvuto; sala ina athari za kiroho. Kwa hiyo, tunasali ‘Ee Mungu! Mponye mgonjwa huyu!’ Pengine Mungu atajibu. Haidhuru nani anasali! Mungu atajibu sala ya kila mtumishi kama sala hiyo ni ya moyo wa dhati. Rehema yake ni kubwa mno, isiyo na mipaka. Yeye hujibu sala za watumishi Wake wote. Hujibu sala za mche huu. Mmea huu husali kwa bidii, ‘Ee Mungu! Niteremshie mvua!’ Mungu hujibu sala hiyo, na mmea hukua. Mungu atamjibu mtu yeyote yule.”[16]**

Ni kawaida kwamba katika sala zetu tunamuomba Mungu atutimizie mahitaji yetu. Hivyo, tunasali kwa ajili ya afya zetu na afya za wapendwa wetu, tunasali kwa ajili ya maendeleo ya kiroho na ya kimwili ya familia zetu, na tunasali kwa ajili ya mwongozo. Tunaomba tupate nguvu, imani, na uthibitisho katika njia ya huduma. Tunapomuomba Mungu, bila shaka tunapaswa tukumbuke kwamba lengo letu maishani ni kupatanisha matakwa yetu na Mapenzi Yake. Kwa hiyo, sharti tuombe ili Mapenzi Yake yatimizwe na kuwa tayari kuyakubali. Kama mtakariri maneno yafuatayo ya ‘Abdu’l-Bahá, yatakuwa kama chanzo cha furaha na matumaini wakati wote:

> **“Ee ewe uliyegeuzia uso wako kuelekea kwa Mungu! Fumba macho yako kwa vitu vingine vyote, na uyafumbulie kwenye milki ya Mtukufu Kabisa. Omba chochote ukitakacho kutoka Kwake pekee; tafuta chochote ukitafutacho kutoka Kwake pekee. Kwa mtazamo mmoja Yeye hujalia taraji mia moja elfu, kwa tazamo la haraka Yeye huponya magonjwa mia moja elfu yasiyotibika, kwa kukubali kwa kichwa Yeye huweka marham kwa kila jeraha, kwa tazamo la mara moja Yeye huachilia mioyo kutoka kwenye pingu za huzuni. Yeye hufanya kama afanyavyo, na je, tuna kimbilio gani? Yeye hutimiza Mapenzi Yake, Yeye huamuru kile apendacho. Basi ni bora zaidi kwako kuinaminisha kichwa chako katika utii, na kuweka tumaini lako katika Bwana Mwenye Rehema-Kabisa.”[17]**

## SEHEMU YA 9

Kutokana na kila kitu tulichojifunza hadi sasa, ni dhahiri kwamba kumgeukia Mungu katika sala ni hitaji muhimu la maisha ya kiroho. Ni tamu jinsi gani hasa kumuomba Mungu mapema baada ya kuamka asubuhi na usiku kabla ya kulala. Muda tunaotumia kusali kila siku na idadi ya sala tuzisemazo hutegemea mahitaji yetu na kiu yetu ya kiroho. Kwa kila nafasi, tunaweza kuchagua kutoka sala nyingi zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá. Hata hivyo, Bahá’u’lláh pia amefunua sala tatu za faradhi za kila siku. Shoghi Effendi husema:

> **“Sala za faradhi za kila siku ni tatu kwa idadi. Ile fupi kabisa ina aya moja tu ambayo sharti itongolewe mara moja tu katika muda wa saa ishirini na nne wakati wa adhuhuri. Ile sala ya kadiri ambayo huanza na maneno, ‘Bwana ni shahidi kwamba hakuna Mungu mwingine ila Yeye,’ sharti itongolewe mara tatu kila siku, asubuhi, adhuhuri na jioni. Ile sala ndefu ambayo ina maelezo mengi zaidi kati ya sala hizo tatu, sharti itongolewe mara moja tu katika muda wa saa ishirini na nne, muda wowote mtu ajisikiapo kufanya hivyo.**

**“Muumini yuko huru kabisa kuchagua sala yoyote ile kati ya sala hizi tatu, lakini anawajibika kutongoa mojawapo, na kulingana na maelekezo yoyote maalumu ambayo inaweza kuambatana nayo.”[18]**

Na huendelea:

**“Sala hizi za faradhi za kila siku, pamoja na zingine chache maalum, kama vile Sala ya Kuponya, Waraka wa Ahmad, zimejaliwa na Bahá’u’lláh nguvu na umuhimu maalum, na kwa hiyo zinapaswa zikubaliwe kama zilivyo na kutongolewa na waumini kwa imani isiyo na shaka na thabiti, ili kupitia hizo waweze kuingia katika mazungumzo ya karibu zaidi na Mungu, na kujifungamanisha wenyewe kikamilifu zaidi na sheria na maagizo Yake.”[19]**

Sala hizi tatu za faradhi zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh husemwa na mtu binafsi. Aina ya sala ya kiusharika ambapo sala ya kila siku ya faradhi hutongolewa katika kikundi kufuatana na kaida fulani haipo katika Imani ya Kibahá’í. Sala kwa ajili ya Marehemu ndiyo sala pekee ya kiusharika iliyoamriwa na sheria ya Kibahá’í. Inapaswa itongolewe na mmoja kati ya wale waliopo kabla ya maziko, wakati kundi lililobaki likiwa limesimama kwa utulivu.

1. Neno “faradhi” humaanisha nini? ________________________________________
   ________________________________________________________________

2. Ni sala ngapi za faradhi za kila siku zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh? ____________
   ________________________________________________________________

3. Je tunapaswa kutongoa sala zote tatu kila siku?_____________________________

4. Kama tukichagua kusema ile Sala Ndefu ya Faradhi, ni mara ngapi tunapaswa kuitongoa kwa kila siku? ______________________________________________

5. Ni mara ngapi tunapaswa kusema, ikiwa tutachagua kutongoa ile Sala ya Wastani ya Faradhi?__________________________________________________________

6. Ni mara ngapi tunapaswa kusema, ikiwa tutachagua kutongoa ile Sala Fupi ya Faradhi?
   ________________________________________________________________

7. Taja baadhi ya sala ambazo zina nguvu maalum: ___________________________
   ________________________________________________________________
   ________________________________________________________________

8. Kariri Sala Fupi ya Faradhi kama hujawahi kufanya hivyo:

**“Nashuhudia, Ee Mungu wangu, kwamba Wewe umeniumba mimi kukujua Wewe na kukuabudu Wewe. Nathibitisha katika wakati huu juu ya unyonge wangu na uwezo Wako, juu ya umasikini wangu na utajiri Wako.**

**“Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Msaada Hatarini, Ajitoshelezaye Mwenyewe.”[20]**

9. Tunashuhudia nini katika sala hii? ________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 10

Tunapaswa tukumbuke kwamba zaidi ya baraka tunazopokea kwa kutii sheria ya sala ya faradhi na chakula tunachopata kutokana na usemaji wa sala zingine kama mtu binafsi, roho zetu zinainuliwa, pale tunaposikia sala zikitongolewa katika mikusanyiko, mikubwa au midogo. Bahá'u'lláh hutuambia:

> **"Kusanyikeni pamoja kwa shangwe na urafiki wa hali ya juu kabisa na tongoeni aya zilizofunuliwa na Bwana mwenye rehema. Kwa kufanya hivyo, milango ya elimu ya kweli itafunguka kwa nafsi zenu za ndani, na kisha mtahisi roho zenu zikijaliwa uthabiti na mioyo yenu ikijawa na furaha angavu."**[21]

Sote tunapata furaha kubwa kutokana na kufahamu kwamba kila mahali ulimwenguni, mikusanyiko ya ibada ambamo marafiki na majirani hukutana pamoja kuzungumza na Mungu inaendelea kuongezeka kwa maelfu. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika:

> **"Mikutano ya ibada ni fursa ambazo roho yoyote inaweza kushiriki, ikivuta pumzi ya manukato ya mbinguni, ikijipatia utamu wa sala, ikitafakari juu ya Neno la Uumbaji, ikiabiriwa kwenye mbawa za roho, na ikizungumza na yule Mpendwa. Hisia za urafiki na kusudi la pamoja hufanyizwa, hasa katika mazungumzo ya hali ya juu ya kiroho ambayo kiasili hutokea katika nyakati hizo na kupitia kwayo 'mji wa moyo wa mwanadamu' unaweza kufunguliwa."**[22]

Tunapohisi kusukumwa kusali, tunasubiri kidogo kwa utulivu kidogo ili kusafisha akili zetu kutokana na mambo ya ulimwengu huu. Wakati tunaposali, tunakazia fikra zetu kwa Mungu. Baada ya kutongoa sala, tunatulia kidogo na hatuanzi kufanya shughuli nyingine papo hapo. Vivyo hivyo ndivyo tunavyofanya tunaposikiliza sala zinazosomwa na wengine katika mkusanyiko. Katika hali kama hizo, tunadumisha hali ya kiibada na kufuatilia maneno kwa ukaribu, kana kwamba sisi ndiyo tunaoyatongoa.

1. Katika hali gani ya kiroho tunapaswa kukusanyika pamoja tunazipotongoa aya za Mungu? ________________________________________________

2. Ni zipi zitakuwa athari za kukusanyika kwetu pamoja kwa ajili ya kutongoa aya za Mungu? ________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

3. Mikutano ya ibada ni nafasi ambazo roho yoyote inaweza

– _________ ,
– _____________________________________________ ,
– _____________________________________________ ,
– _____________________________________________ ,
– ________________________________________________________________ , na
– ________________________________________________________________ .

4. Ni hisia gani hufanyizwa wakati wa mikutano ya ibada? ________________________

___________________________________________________________________________

5. Ni athari zipi za mazungumzo yaliyoinuliwa kiroho ambazo kwa kawaida hutokea wakati wa mikutano ya ibada? ________________________________________________

___________________________________________________________________________

6. Andika maneno machache kuhusu hali ya heshima tunayopaswa kuonesha tunaposali, iwe peke yetu au katika mkusanyiko.

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Kitengo cha kwanza cha kitabu hiki kilijikita juu ya desturi ya kusoma vifungu kutoka Maandiko kila siku na kutafakari juu ya maana zake. Hapa umetafakari juu ya umuhimu wa sala na matokeo yake umeimarisha desturi ya kusali kila siku. Sehemu iliyotangulia imekufahamisha juu ya umuhimu wa ibada ya pamoja. Yote uliyojifunza hadi sasa yamekuandaa kufanya ukihitaji, kitendo cha kwanza kwenye njia ya huduma: kukaribisha mkutano wa ibada.

Kama hatua ya awali, pengine ungependa kukariri sala kadhaa na kutafuta fursa ya kushiriki na marafiki wachache. Wakati huo huo, unaweza kuhakikisha kwamba unahudhuria angalau mkutano mmoja wa ibada wa jumuiya yako na unahesabika miongoni mwa wasaidizi wake wenye shauku. Hatimaye, basi, unaweza kuamua kukirimu mkutano wa ibada wewe mwenyewe, ukiwaalika marafiki zako, wana-familia na majirani kukusanyika mara kwa mara

kwa ajili ya ibada na urafiki. Ni kawaida kwa washiriki wawili au watatu wa kozi hii kuanzisha mkutano wa ibada kama huo kwa pamoja.

Kama unavyoweza kudhani, hakuna fomyula za jinsi mkutano wa ibada unavyopaswa kuandaliwa. Lakini ni dhahiri kwamba mkusanyiko huo ni wa marafiki ambapo sala husomwa, vifungu kutoka Maandiko husomwa, na mazungumzo yainuayo hufanyika—yote yakifanyika katika mazingira dhahiri ya kiroho. Je, unaweza kusema maneno machache kuhusu kila moja ya mawazo yafuatayo katika muktadha wa kukaribisha mkutano wa ibada?

Kutuma mialiko kwa moyo mkunjufu na wa upendo: ___________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

Kuandaa mazingira ya kirafiki: ___________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

Kudumisha mazingira yenye adhama: ______________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

Kuendeleza urafiki wenye furaha: _________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

Kuhamasisha mazungumzo yainuayo ya kiroho: ______________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

## MAREJELEO


1. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983, chapisho la 2017), XLIII, aya. 4, uk. 105. (toleo la Kiingereza)

2. Bahá'u'lláh, katika *Uaminifu: Mkusanyo wa Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá'í*, zilizokusanywa na Idara ya Utafiti Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (London: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1987), na. 21, uk. 5. (toleo la Kiingereza)

3. *Mwito wa Mpendwa Mtakatifu: Vitabu vya Mafumbo Vilivyoteuliwa vya Bahá'u'lláh* (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu, 2018), na. 2.43, uk. 31. (toleo la Kiingereza)

4. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa 5 Mei 1912, na kuchapishwa katika *The Promulgation of Universal Peace: Talks Delivered by 'Abdu'l-Bahá during His Visit to the United States and Canada in 1912* [Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo yaliyoyolewa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa ziara Yake huko Marekani na Canada mnamo mwaka 1912] (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), uk. 127. (toleo la Kiingereza)

5. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá'í wa Tanzania, chapisho la 2017), Kiarabu na 13, uk. 5.

6. Kutoka barua ya 8 Desemba 1935 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, imechapishwa katika *Sala na Maisha ya Kiibada: Makusanyo ya Dondoo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh, Báb, na 'Abdu'l-Bahá na Barua za Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, zilizokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2019), na. 71, uk. 31. (toleo la Kiingereza)

7. Maneno ya 'Abdu'l-Bahá, yamenukuliwa na J. E. Esslemont, *Bahá'u'lláh na Wakati Mpya: Utambulisho wa Imani ya Kibahá'í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, chapisho la 2017), uk. 106. (toleo la Kiingereza)

8. Kama hapo juu.

9. Bahá'u'lláh, katika *Sala za Kibahá'í: Mateuzi ya Sala Zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb, na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2002, chapisho la 2017), ku. 7–8. (toleo la Kiingereza)

10. Kama hapo juu, uk. 9.

11. Maneno ya 'Abdu'l-Bahá, yamenukuliwa katika *Nyota ya Magharibi*, juz. 8, na. 4 (17 Mei 1917), uk. 41. (toleo la Kiingereza)

12. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXVI, aya. 2, uk. 334; pia katika *Sala za Kibahá'í*, uk. iii.

13. Bahá'u'lláh, katika *Sala za Kibahá'í*, uk. 8–9.

14. Kama hapo juu, uk. 12.

15. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala na Maisha ya Kiibada*, na. 24, uk. 7.

16. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá 5 Agosti 1912, yamechapishwa katika *The Promulgation of Universal Peace* [Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu], uk. 345.

17. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010, chapisho la 2015), na. 22.1, ku. 75–76. (toleo la Kiingereza)

18. Kutoka barua ya 10 Januari 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, imechapishwa katika *Sala na Maisha ya Kiibada*, na. 61, uk. 23.

19. Kutoka barua ya 10 Januari 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, ikinukuliwa katika *Sala za Kibahá’í*, uk. 301.

20. Bahá’u’lláh, katika *Sala za Kibahá’í*, uk. 4.

21. Bahá’u’lláh, katika *Sala na Maisha ya Kiibada*, na. 68, uk. 27.

22. Kutoka ujumbe wa 29 Desemba 2015, umechapishwa katika *Muundo wa Kiutendaji: Jumbe Zilizoteuliwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Nyenzo za Ziada, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2017), na. 35.49, uk. 232.



# Uhai na Kifo

## Kusudi

Kutambua kwamba maisha hayajumuishi
tu mabadiliko na nasibu za ulimwengu huu
bali hupata maana yake ya kweli katika
maendeleo ya roho

## SEHEMU YA 1

Roho ya mwanadamu imetukuzwa juu ya vitu na ulimwengu wa kimwili. Katika mojawapo ya mazungumzo Yake, 'Abdu'l-Bahá hueleza:

> **"Miili hii ya vumbi imeundwa na atomu; pale atomu zinapoanza kutengana kuoza huanza kutokea, kisha huja kile tunachokiita kifo.…**
>
> **"Kwa roho ni tofauti. Roho siyo muunganiko wa elementi, haijaundwa kwa atomu nyingi, ni kile kitu kisichogawanyika na kwa hiyo cha milele. Haimo kabisa katika utaratibu wa muumbo wa kimwili; ni ya milele."[1]**

1. "Kuundwa" humaanisha nini? ____________________________________________

2. Je, roho ya mwanadamu imeundwa na elementi mbalimbali, kama livyo miili ya vumbi?

   ____________________________________________________________________

3. Je, roho ya mwanadamu ni kitu cha kimwili? ________________________________

## SEHEMU YA 2

Barua moja iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi hueleza kwamba "roho ya mtu huanza pale mimba inapotungwa".[2] Ikijibu swali kuhusu maana ya "utungaji mimba", Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutanabahi:

> **"Hakuna chochote kilichopatikana kutoka maandiko ya Kibahá'í ambacho hufafanua wazi wazi wakati wa kibiolojia na asili ya tukio lililoelezwa kama 'utungaji mimba'. Matumizi ya istilahi hii katika muktadha wa kitabibu pia yanadhihirika kuwa siyo sahihi. Kwa hakika, uelewa mmoja wa utungaji wa mimba ni kwamba unaenda sambamba na urutubishaji wa yai, tena mwingine ni ule unaotokeo baada ya urutubishaji wa yai na upandikizaji, mwanzo wa uja-uzito. Hivyo pengine haiwezekani kujua ni lini uhusiano wa roho na umbo la kimwili hutokea, na maswali kama hayo hayawezi kujibika kwa fikra ya mwanadamu au uchunguzi kwa kuwa yanahusu siri za ulimwengu wa kiroho na asili ya roho yenyewe."[3]**

1. Roho ya mwanadamu huanza kutokea lini? __________________________________

   ____________________________________________________________________

2. Je, istilahi "utungaji mimba" huelezea tukio halisi la kibiolojia? ________________

## SEHEMU YA 3

Uhusiano kati ya roho na mwili siyo wa kimwili; roho haingii wala kutoka mwilini na haichukui nafasi ya kimaumbile. Uhusiano wake na mwili unafanana na ule wa mwanga na kioo kinachouakisi. Mwanga unaoonekana katika kioo haumo ndani mwake. Vivyo hivyo, roho haimo ndani ya mwili. Kama 'Abdu'l-Bahá anavyoeleza,

> **"roho yenye mantiki, au roho ya mtu, haiishi kupitia mwili huu kiasili—ndiyo kusema, haiingii ndani yake; kwani miili ina sifa za kiasili na kupokea, na roho yenye mantiki imetakasika juu ya hili. Kwa kuanza kamwe haingii ndani ya mwili huu, kwamba ihitaji makazi mengine pindi inapouacha mwili. Hapana, uhusiano wa roho na mwili ni kama uhusiano wa taa hii na kioo. Kama kioo kimeng'arishwa vizuri na kwa ukamilifu, mwanga wa taa huonekana ndani mwake, na kama kioo kimevunjika au kimefunikwa na vumbi, mwanga utabaki umefichika."**[4]

1. Jaza nafasi zilizo wazi katika sentensi hapa chini.

   a. Roho yenye mantiki, au ___________________ , haiishi kupitia mwili huu kiasili mwili kiasili—ndiyo kusema, roho ________________________________ .

   b. _________________________________ au roho ya mtu, haiingii mwilini kwani _______________________ na roho yenye mantiki _______________________ .

   c. Kwa kuanza, roho kamwe _________________________, kwamba ihitaji makazi mengine pindi inapouacha, _____________________ .

   d. Uhusiano wa roho na mwili ni kama uhusiano wa ________________________ .

   e. Kama kioo kimeng'arishwa vizuri na kwa ukamilifu, _______________________ huonekana ndani mwake.

   f. Kama kioo kimevunjika au kufunikwa na vumbi __________________________ .

2. Kwa kuzingatia yale tuliyokwishajifunza mpaka sasa, amua ikiwa yafuatayo ni kweli:

   _____ Roho haitoki katika ulimwengu wa kimwili.
   _____ Roho imo ndani ya mwili.
   _____ Mwili ni mmiliki wa roho.
   _____ Roho ni ya milele.
   _____ Mtu huanza pale roho inapojihusisha yenyewe na kiinitete.
   _____ Maisha huanza pale mtu anapozaliwa katika ulimwengu huu.
   _____ Maisha ya kimwili ya mtu huendelea baada ya kifo.
   _____ Maisha hujumuisha mambo ambayo hututokea kila siku.

3. Tumia taswira ya mwanga na kioo kuelezea uhusiano uliopo kati ya roho na mwili:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 4

Kuna uhusiano maalum sana kati ya roho na mwili ambavyo kwa pamoja humfanya mwanadamu. Uhusiano huu hudumu tu kwa muda mfupi wa maisha ya umauti. Wakati uhusiano huu ukikoma, kila kimoja hurudi katika sehemu yake ya asili—mwili kwenye ulimwengu wa vumbi, na roho kwenye malimwengu ya kiroho ya Mungu, ambako huendelea milele. 'Abdu'l-Bahá hueleza:

> **"Roho ya mwanadamu ina mwanzo lakini haina mwisho: Hudumu milele."[5]**

Katika mojawapo ya mazungumzo Yake, Yeye hufafanua:

> **"Roho haiuhitaji mwili, lakini mwili unaihitaji roho, la sivyo hauwezi kuishi. Roho inaweza kuishi bila mwili, lakini mwili bila roho hufa."[6]**

Na Mlinzi hueleza:

> **"Kuhusu roho ya mwanadamu: Kulingana na Mafundisho ya Kibahá'í roho ya mtu huanza pamoja na utungo wa kiinitete cha mwanadamu, na huendelea kukua na kupita katika hatua zisizo na mwisho za uhai baada ya kutengana kwake na mwili. Hivyo, maendeleo yake hayana kikomo."[7]**

1. Ukiwa na nukuu hiyo hapo juu akilini, jibu maswali yafuatayo:

   a. Je, mwili unaihitaji roho?______________________________

   b. Je, roho inauhitaji mwili?______________________________

   ______________________________________________

   c. Nini hutokea kwenye uhusiano kati ya mwili na roho tunapofariki?__________

   ______________________________________________

   d. Nini hutokea kwa roho baada ya kifo? ________________________

   ______________________________________________

   e. Ni kwa muda gani maendeleo ya roho hudumu?___________________

   ______________________________________________

f. Lini maisha hufikia kikomo? ________________________________________

________________________________________________________________

2. Amua ni yapi kati ya yafuatayo hukubaliana na kile ambacho tumekwishajifunza katika sehemu hizi:

_____ Kifo ni adhabu.

_____ Uhusiano kati ya mwili na roho hudumu kwa muda wa maisha ya umauti tu.

_____ Mwili una uwezo wa kuendelea milele.

_____ Roho itaendelea milele.

_____ Kifo ni mwisho wa uhai.

_____ Kutakuwa na siku ya hukumu ambapo miili yetu itafufuka.

_____ Wakati wa kifo, roho ina uhuru zaidi kuliko ilivyokuwa kabla.

_____ Maisha huishia na kifo.

_____ Tunapaswa kuogopa kifo.

_____ Chakula, mavazi, burudani ni vya muhimu kwa roho.

_____ Roho huchoka kadiri mwili unavyotumia nguvu zake.

_____ Roho haiathiriwi na maradhi wala udhaifu wa mwili.

_____ Mwanadamu ataendelea kuwa na mahitaji ya kimwili baada ya kifo.

## SEHEMU YA 5

Tumeona kwamba roho haichukui nafasi ya kimaumbile na haitendi kulingana na sheria za asili, kama vitendavyo vitu vya kimwili. Roho huleta athari zake ulimwenguni kupitia uwakala wa mwili, lakini hii siyo njia pekee ambayo kwayo roho huonesha nguvu zake. Bahá'u'lláh hutamka:

**"Kwa kweli Nasema, roho ya mwanadamu imetukuzwa zaidi ya vyote vilivyo huru na visivyo huru. Imetulia na bado inapaa; inajongea na bado imelulia."[8]**

Na 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

**"Jua kwamba athari na muonekano wa roho ya mwanadamu ni wa aina mbili; yaani, roho ya mwananadamu ina namna mbili za utendaji na uelewa. Namna moja ni kupitia uwakala wa viungo vya mwili na ogani. Hivyo inaona kwa macho; inasikia kwa masikio; inaongea kwa ulimi.…**

**"Namna nyingine ya athari ya roho na utendaji ni bila viungo na ogani hizi za mwili."[9]**

1. Jaza katika nafasi zilizo wazi za sentensi zifuatazo:

   a. Roho ya mwanadamu imetukuzwa zaidi ya vyote _____________ na _________ .

   b. _____________________ na bado _______________________ .

   c. _____________________ na bado _______________________ .

2. Eleza namna mbili ambazo kwazo roho huonesha na kuleta athari zake katika ulimwenguni huu: ____________________________________________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

3. Je, unaweza kutoa mifano ya athari na utendaji wa roho bila viungo vya mwili?

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Sasa, kulingana na majadiliano ya sehemu zilizotangulia, soma kifungu kifuatacho kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

> **"Jua kwamba roho ya mwanadamu imetukuzwa juu ya, na i huru na udhaifu wote wa kimwili na kiakili. Kwamba mgonjwa huonesha dalili za udhaifu ni kutokana na vizuizi vinavyojiweka katikati ya roho yake na mwili wake, kwa kuwa roho yenyewe hubakia bila kuathiriwa na maradhi yoyote ya kimwili. Fikiria mwanga wa taa. Ingawa kitu cha nje kinaweza kukinga mng'ao wake, mwanga wenyewe huendelea kung'aa kwa nguvu zisizopungua, vivyo hivyo, kila maradhi yanayoushambulia mwili wa mwanadamu ni kizuizi kinachoizuia roho kudhihirisha uwezo na nguvu zake za kiasili. Inapouacha mwili, hata hivyo, itaonesha ule ukuu na kufunua ile athari kiasi kwamba hakuna nguvu duniani iwezayo kulingana nayo. Kila roho safi, iliyotakasika na takatifu itajaliwa uwezo mkubwa mno, na itashangilia kwa furaha kubwa kabisa."[10]**

1. Elezea kwa maneno yako mwenyewe jinsi roho inavyobakia bila kuathiriwa na udhaifu wa mwili au akili, na kile kitakachodhihirika wakati wa kutengana kwake na mwil.

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

2. Je, tutaendelea kudumisha sifa zetu baada ya kifo cha miili yetu ya vumbi? ________

## SEHEMU YA 7

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Na sasa, kuhusu swali lako juu ya roho ya mtu na kuendelea kuishi kwake baada ya kifo. Fahamu wewe kwa ukweli kwamba roho, baada ya kutengana na mwili, itaendelea kwenda mbele mpaka ifikie ukaribu wa Mungu, katika kiwango na hali ambayo mabadiliko ya nyakati na karne, hata mageuzi na nasibu za ulimwengu huu haziwezi kubadilisha. Itadumu kadiri Ufalme wa Mungu, enzi Yake, milki Yake, na uwezo Wake vitakavyodumu. Itadhihirisha ishara za Mungu na sifa zake, na itafunua wema wa upendo wa baraka Zake."**[11]

1. Ni kwa muda gani roho itaendelea kwenda mbele baada ya kutengana na mwili? ___

_______________________________________________________________

2. Ikiwa katika hali gani roho itaendelea na safari yake kwenda mbele ya Mungu? ____

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

3. Zipi baadhi ya sifa na ishara ambazo roho itaonesha ikiwa katika hali hiyo? ________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

4. Kulingana na yale tuliyokwishasoma hadi sasa, amua ikiwa yafuatayo ni kweli:

______ Ufalme wa Mungu utadumu milele.

______ Roho ina uwezo wa kudhihirisha sifa za Mungu.

______ Sala tuzisemazo kwa ajili ya marehemu haziathiri maendeleo ya roho zao.

______ Kamwe roho haina ukomo wa kuishi.

## SEHEMU YA 8

Bahá'u'lláh husema:

**"Fahamu wewe kwamba kila sikio sikivu, likiwekwa safi na bila kunajisiwa, lazima nyakati zote na kutoka kila upande, lisikie sauti inenayo maneno haya matakatifu: 'Kwa kweli, sisi ni wa Mungu na Kwake tutarejea.' Siri za kifo cha kimwili cha mwanadamu na za kurejea kwake hazijafichuliwa, na bado zimebaki bila kusomwa.…**

**"Kifo humpa kila muumini mwaminifu kikombe ambacho kwa kweli ndiyo uhai wenyewe. Hujalia shangwe, na ni mchukuzi wa furaha. Hutoa zawadi ya uzima wa milele.**

**"Na kwa wale ambao wameonja tunda la maisha ya duniani ya mwanadamu, ambalo ni utambuzi wa Mungu mmoja wa kweli, utukuzwe utukufu Wake, maisha yao baada ya hapa yatakuwa ya namna ambayo Hatuwezi kuelezea. Elimu hiyo anayo Mungu pekee, Bwana wa malimwengu yote."[12]**

**"Ewe Mwana wa Mwenye enzi! Nimekifanya kifo kuwa mjumbe wa furaha. Kwa nini basi unahuzunika? Niliifanya nuru ili iangazie utukufu wake juu yako. Kwa nini unajificha kutoka kwayo?"[13]**

1. Zipi kati ya kauli zifuatazo ni za kweli?

   _____ Roho ya mwanadamu hutoka kwa Mungu na itarejea Kwake.

   _____ Elimu yote ya uhai baada ya kifo anayo Mungu.

   _____ Kwa muumini mwaminifu, kifo ni uhai.

   _____ Kifo ni mchukuzi wa furaha.

   _____ Siri za kifo zinajulikana na wote.

   _____ Tunapaswa kuthamini baraka za maisha walakini tusiogope kifo, kwani ni mjumbe wa furaha.

   _____ Siyo muhimu kwetu kujua kuhusu uhai na kifo.

2. Sasa, kwa kuzingatia kile tulichojifunza katika sehemu hizi, andika aya fupi kuhusu uhai, kifo, mwili na roho.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 9

'Abdu'l-Bahá hueleza:

**"Mwanzoni mwa uhai wake mwanadamu alikuwa katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, ambamo alikuza uwezo na ustahiki wa kuendelea katika ulimwengu huu. Vipawa vilivyohitajika kwa ajili ya ulimwengu huu alivipata katika ulimwengu ule. Alihitaji macho katika ulimwengu huu; aliyapata katika ulimwengu wa tumbo la uzazi. Alihitaji masikio katika ulimwengu huu; aliyapata huko. Vipawa vyote vilivohitajika katika ulimwengu huu alivipata katika ulimwengu wa tumbo la uzazi. Katika ulimwengu ule aliandaliwa kwa ajili ya ulimwengu huu, na alipoingia katika ulimwengu huu, alijikuta kwamba ana vipawa vyote vinavyohitajika na alipata viungo na ogani zote zinazohitajika kwa ajili ya maisha haya, katika ulimwengu ule. Inamaanisha kwamba katika ulimwengu huu pia lazima ajiandae kwa ajili ya ulimwengu ujao. Kile ambacho yeye anakihitaji katika ulimwengu wa Ufalme lazima akipate na kukiandaa hapa. Kama vile alivyopata vipawa vinavyohitajika kwa ajili ya ulimwengu huu katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, hivyo, vivyo hivyo, sharti ajipatie kile ambacho atakihitaji katika ulimwengu wa Ufalme—yaani, vipawa vyote vya mbinguni—katika ulimwengu huu."[14]**

1. Amua kama yafuatayo ni kweli au la:

    _____ Vipawa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya ulimwengu huu vinapatikana katika ulimwengu wa tumbo la uzazi.

    _____ Hakuna haja ya mtu kujiandaa kwa ajili ya maisha katika ulimwengu ujao.

    _____ Kile tunachokihitaji katika ulimwengu wa Ufalme lazima kipatikane huko.

    _____ Kusudi la maisha haya ni kujipatia vipawa vinavyohitajika kwa ajili ya maisha katika ulimwengu ujao.

    _____ Maisha ya kweli huanzia pale mtu anapofariki na kwenda kwenye Ufalme mtakatifu.

    _____ Maisha ya kweli huanzia katika ulimwengu huu na huendelea baada ya kifo cha kimwili.

2. Ni upi baadhi ya uwezo ambao mwanadamu huupata katika ulimwengu wa tumbo la uzazi? ______________________________

______________________________

3. Ni yapi baadhi ya majaliwa ambayo sharti yapatikane hapa kwa ajili ya maisha baada ya kifo? ______________________________

______________________________

## SEHEMU YA 10

Bahá'u'lláh husema:

**"Wajibu kamili wa mtu katika Siku hii ni kuifikia ile sehemu ya mafuriko ya neema ambayo Mungu humimina kwa ajili yake. Asiwepo yeyote, kwa hiyo, atakayefikiria juu ya ukubwa au udogo wa chombo. Sehemu ya baadhi inaweza kuwa katika kiganja cha mkono wa mtu, sehemu ya wengine inaweza kujaza kikombe, na wengine hata kipimo cha galoni."**[15]

1. Kufuatana na teuzi la hapo juu, jibu maswali yafuatayo:

   a. Ni upi wajibu wa kila mtu katika Siku hii? ______________________________

   ______________________________

   b. Ni zipi baadhi ya baraka ulizozipokea kutoka kwa Mungu? ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   c. Neno "chombo" katika teuzi la hapo juu hurejelea nini? ______________________________

   ______________________________

   d. Kwa nini hatupaswi kufikiria "ukubwa au udogo" wa uwezo tuliojaliwa? ______

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   e. Ni vipi baadhi ya vitu vinavyotuzuia kupokea sehemu yetu ya neema ya Mungu?

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

2. Yapi kati ya yafuatayo ni kweli?

_____ "Ukubwa au udogo" wa uwezo wetu hurejelea jinsi tulivyo wajuzi.

_____ Kumtumikia Mungu, tunahitaji kusahau udhaifu wetu na kuweka imani yetu yote Kwake.

_____ Tusipokuza uwezo ambao Mungu ametujalia, roho zetu zitakuwa dhaifu tutakapofika katika ulimwengu ujao.

## SEHEMA YA 11

Bahá'u'lláh hueleza:

**"Umeniuliza Mimi kuhusu asili ya roho. Jua, kwa kweli, kwamba roho ni ishara ya Mungu, kito cha mbinguni ambacho uhalisi wake hata wale walioelimika kabisa wameshindwa kuufahamu, na ambayo siri yake hakuna akili, hata iwe ipenyezayo jinsi gani, inayoweza daima kutumaini kuivumbua. Ni ya kwanza miongoni mwa vitu vyote vilivyoumbwa kutangaza ubora wa Muumba wake, ya kwanza kuutambua utukufu Wake, kushikilia kwenye ukweli Wake, na kumsujudia Yeye."**[16]

1. Jaza nafasi zilizo wazi katika sentensi zifuatazo:

a. Roho ni ___________ ya Mungu.

b. Roho ni kito cha ________________ ambacho ____________________ hata wale wenye elimu ya juu kabisa wameshindwa kuufahamu, na ambao fumbo lake hakuna akili, hata iwe ipenyezayo jinsi gani, inayoweza daima kutumaini _____________ .

c. Roho ni ______________________________ kutangaza ____________________ .

d. Roho ni ya kwanza _____________________ utukufu wa Mungu.

e. Roho ni ya kwanza ________________________ ukweli wa Mungu.

f. Roho ni ya kwanza __________________________________ Mungu.

2. Yapi miongoni mwa yafuatayo ni kweli?

_____ "Kuvumbua" humaanisha kuelewa.

_____ Miongoni mwa vitu vyote vilivyoumbwa, cha kwanza kumtambua Mungu ni akili ya mwanadamu.

_____ "Ipenyezayo" humaanisha kali.

_____ Mtu aliyeelimika huelewa fumbo la roho.

_____ Ni wanafalsafa wakuu pekee ndio wanaoweza kuutangaza ubora Mungu.

_____ Siyo muhimu kufikiria kuhusu roho kwa sababu kamwe hatutaweza kuielewa.

## SEHEMU YA 12

Bahá'u'lláh husema:

**"Ninyi ni kama ndege anayepaa, kwa uwezo wote wa mabawa yake yenye nguvu, na kwa ujasiri kamili na wenye furaha, kwenye mapana ya mbingu, hadi, akisukumwa kutosheleza njaa yake, huyageukia kwa hamu sana maji na udongo wa ardhi iliyo chini yake, na, akishanaswa katika wavu wa tamaa yake, hujikuta asiyeweza kurudia kupaa kwake kwenda kwenye milki alizotoka. Akiwa hana nguvu ya kukung'uta mzigo unaolemea mabawa yake yaliyochafuka, ndege huyo, ambaye alikuwa mkazi wa mbinguni, sasa hulazimika kutafuta makao kwenye mavumbi. Kwa hiyo, Enyi watumishi Wangu, msiyachafue mabawa yenu kwa udongo wa upotovu na tamaa za bure, na msiyaache yachafuliwe kwa vumbi la husuda na chuki, ili msizuiwe kupaa katika mbingu za elimu Yangu takatifu."**[17]

1. Kamilisha sentensi za hapa chini.

   a. Ndege ambaye Bahá'u'lláh humzungumzia katika teuzi hili ni ______________ .

   b. Ndege huyu ni mkazi wa ___________________________ .

   c. Kama mabawa yake yakichafuliwa ndege huyo hulazimika kutafuta makazi yake katika _____________ .

2. Sasa jibu maswali yafuatayo:

   a. Jinsi gani "mabawa" ya roho "huchafuka"? ______________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   b. Ni ipi baadhi ya mizigo ambayo, kama "maji na udongo wa ardhi", huyaelemea mabawa ya roho? ____________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   c. Ni yapi baadhi ya mambo ambayo yanaweza kutuzuia kupaa katika mbingu za elimu takatifu? ____________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   d. Kwa nini roho ibadili makazi yake ya mbinguni kwa vumbi la ulimwengu huu?

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

3. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

_____ Mwambatano na mambo ya kiulimwengu huzuia maendeleo yetu ya kiroho.

_____ Upotovu na tamaa zetu za bure hutuzuia kupaa kwenye mbingu za elimu takatifu.

_____ Husuda na chuki ni desturi za kiasili za mwanadamu na haziielemei roho.

_____ Tunaweza kujiondolea wenyewe mizigo ambayo hutuzuia kupaa katika mapana ya mbingu kwa kujitenga na mambo ya ulimwengu huu.

_____ Makazi ya roho ni katika ulimwengu huu.

## SEHEMU YA 13

Bahá'u'lláh husema:

**"Baada ya kuuumba ulimwengu na vyote viishivyo na kutembea humo, Yeye, kupitia utendaji wa moja kwa moja wa Mapenzi Yake yasiyozuilika na yenye mamlaka, Alichagua kumjalia mwanadamu heshima na uwezo wa kipekee wa kumjua Yeye na kumpenda Yeye—uwezo ambao sharti ufikiriwe kama msukumo unaofanyiza na kusudi la kimsingi la muumbo mzima.… Juu ya uhalisi wa ndani kabisa wa kila kiumbe Yeye amemulika mojawapo ya majina Yake, na kulifanya mpokezi wa utukufu wa mojawapo ya sifa Zake. Juu ya uhalisia wa mtu, walakini, Yeye amekazia mng'ao wa majina na sifa Zake zote, na kuufanya kioo cha Nafsi Yake Mwenyewe. Pekee kati ya viumbe vyote mwanadamu ameteuliwa kwa upendeleo mkuu kama huo, baraka inayodumu hivyo."[18]**

1. Jaza katika nafasi zilizopo hapa chini.

   a. Mungu alichagua kumjalia mwanadamu heshima na uwezo wa kipeke wa ________________________________________ .

   b. Juu ya uhalisi wa ndani kabisa wa ____________ kiumbe Mungu alimulika ________________________________ , na kulifanya mpokezi wa utukufu wa ____________________________________________________________ .

   c. Juu ya uhalisi wa mwanadamu, Yeye amekazia _________________________ , na kuufanya kioo cha ____________________________________________ .

2. Sasa jibu maswali yafuatayo:

   a. Je, unaweza kutaja baadhi ya sifa za Mungu? __________________________
   ____________________________________________________________
   ____________________________________________________________

b. Ni zipi baadhi ya sifa za Mungu mbazo roho ya mwanadamu inaweza kuziakisi?

________________________________________________________

________________________________________________________

c. Jinsi gani sifa hizi zinaweza kudhihirishwa? ______________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

d. Mwanadamu ameteuliwa kwa upendeleao gani maalum? ____________________

________________________________________________________

________________________________________________________

3. Ni yapi kati ya yafuatayo ni kweli?

_____ Mwanadamu hana tofauti na muumbo mwingine wote.

_____ Uwezo wa kumjua Mungu na kumpenda Yeye ni msukumo ufanyizao na kusudi la kimsingi la muumbo mzima.

_____ Uhalisia wa kila kiumbe ni mpokezi wa mojawapo ya sifa za Mungu.

_____ Roho ya mwanadamu inaweza kuakisi sifa zote za Mungu.

## SEHEMU YA 14

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Nguvu hizi ambazo kwazo Nyota ya Mchana ya baraka za Mungu na Chanzo cha mwongozo wa mbinguni zimeujalia uhalisia wa mtu, hata hivyo, zikiwa na uwezo fiche ndani mwake, kama vile mwali ulivyofichika ndani ya mshumaa na mionzi ya mwanga ilivyo na uwezo uliofichika ndani ya taa. Wangavu wa nguvu hizi unaweza kutiwa giza na tamaa za kidunia kama vile mwanga wa jua unavyoweza kufichwa chini ya vumbi na uchafu unaokifunika kioo. Si mshumaa wala taa vinaweza kuwashwa kupitia juhudi zao bila kusaidiwa, wala haiwezekani kamwe kioo kujisafisha uchafu wake. Ni wazi na dhahiri kwamba hadi pale moto uwashwapo taa haiwezi kamwe kuwaka, na vinginevyo uchafu umeondolewa kwenye uso wa kioo kamwe hakiwezi kuonesha taswira ya jua wala kuakisi mwangaza na utukufu wake."[19]**

1. Nini maana ya neno "uwezo fiche"? ______________________________________

____________________________________________________________

2. Ni vipi baadhi ya vipawa ambavyo vimejificha katika roho ya mwanadamu? ______

____________________________________________________________

____________________________________________________________

3. Taa ina uwezo gani uliofichika?__________________________________________

4. Kioo kina uwezo gani uliofichika?________________________________________

5. Unapaswa kufanya nini ili taa iweze kutoa mwanga? __________________________

____________________________________________________________________

6. Unapaswa kufanya nini ili kioo kiweze kuakisi mwanga?______________________

____________________________________________________________________

7. Je, taa na kioo vinaweza kudhihirisha vyenyewe uwezo wao uliojificha?__________

8. Tunawezaje kuhusianisha mifano hii miwili na hali ya roho ya mwanadamu? ______

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

9. Nani anaweza kuifanya roho ya mwanadamu idhihirishe uwezo wake uliofichika?

____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 15

Bahá'u'lláh hutamka:

> **"Mlango wa maarifa ya Yule Mkale daima umekuwa na utaendelea milele kuwa, umefungwa mbele ya nyuso za wanadamu. Hakuna ufahamu wa yeyote kamwe utafikia kitala Chake kitakatifu. Kama ishara ya rehema Yake, walakini, na kama uthibitisho wa wema Wake wa upendo, Yeye amewadhihirishia wanadamu Nyota za Mchana za mwongozo Wake mtakatifu, Alama za umoja Wake mtakatifu, na ameamuru kuwajua Viumbe hawa Waliotakasika kama kuijua Nafsi Yake Mwenyewe. Yeyote awatambuaye Wao amemtambua Mungu. Yeyote asikilizaye na kujali mwito Wao, amesikiliza na kujali sauti ya Mungu, na yeyote ashuhudiaye ukweli wa Ufunuo Wao ameshughudia ukweli wa Mungu Mwenyewe. Yeyote ageukiaye mbali kutoka kwao, amegeukia mbali kutoka kwa Mungu, na yeyote asiyewaamini Wao, hajamwamini Mungu. Kila mmoja Wao ni Njia ya Mungu ambayo huunganisha ulimwengu huu na milki za juu, na Kipimo cha Ukweli Wake kwa kila mmoja katika falme za duniani na mbinguni. Wao ni Wadhihirishaji wa Mungu miongoni mwa watu, uthibitisho wa Ukweli Wake, na ishara za Utukufu Wake."**[20]

1. Ukiwa na teuzi la hapo juu akilini, jibu maswali yafuatayo:

   a. Je, inawezekana kwetu kumjua Mungu moja kwa moja? ____________________

b. Jinsi gani, basi tunaweza kumjua Mungu? ______________________________

______________________________________________________________

c. Je, unaweza kutaja baadhi ya Nyota za Mchana za mwongozi mtakatifu? ______

______________________________________________________________

d. Wale waliowasikiliza Wadhihirishaji wa Mungu wamesikiliza sauti ya Nani?

______________________________________________________________

e. Tunamkengeukia Nani tunapopuuzia mwito wa Wadhihirishaji wa Mungu? ____

______________________________________________________________

2. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Mlango wa maarifa ya Yule Mkale daima umekuwa na utaendelea milele kuwa, ______________________________________________________________ .

b. Hakuna ufahamu wa yeyote kamwe utafikia ______________________________ .

c. Mungu aliwatuma Wadhihirishaji Wake kama ishara ya ____________ Yake na kama uthibitisho wa _______________________________________ .

d. Kuwajua Wadhihirishaji wa Mungu ni sawa na __________________________ ____________________________________ .

e. Yeyote awatambuaye Wao ame ________________________________________ .

f. Yeyote asikilizaye mwito Wao ame _____________________________________ .

g. Kila mmoja Wao ni Njia ya Mungu ambayo ______________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________ .

3. Yapi kati ya yafuatayo ni kweli?

_____ Tunaweza kukua kiroho kupitia juhudi zetu pekee.

_____ Mungu ametupa akili, na inatosha kwa ajili ya maendeleo yetu.

_____ Tutaendelea kiroho kwa kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu na hatutahitaji kufanya juhudi zaidi.

_____ Tutaweza kuendelea kiroho kwa kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu na kufanya juhudi kuishi kufuatana na mafundisho Yake.

_____ Tunaweza kumjua Mungu moja kwa moja.

_____ Mwanadamu anaweza kuwa kama Mungu tu.

_____ Mungu ametukuka juu zaidi ya ufahamu wa mwanadamu.

_____ Tunaposikiliza maneno ya Mdhihirishaji wa Mungu, tunasikiliza Sauti ya Mungu.

## SEHEMU YA 16

Bahá'u'lláh husema:

**"Mitume na Wajumbe wa Mungu wameteleshwa kwa kusudi moja tu la kuiongoza jamii ya wanadamu katika Njia iliyonyoka ya Ukweli. Kusudi la msingi la ufunuo Wao limekuwa kuwaelimisha watu wote, ili waweze, ifikapo saa ya kifo, kupaa, wakiwa katika usafi na utakaso wa hali juu kabisa na kwa kujitenga kikamilifu, kuelekea kiti cha enzi cha Aliye Juu Kabisa."**[21]

Na katika kifungu kingine, Yeye husema:

**"Mwamadamu ni Talasimu kuu kabisa. Ukosefu wa elimu inayofaa, walakini, umemnyima kile ambacho kwa asili anacho. Kwa neno moja lililotoka kwenye kinywa cha Mungu aliumbwa; na kwa neno lingine zaidi aliongozwa kutambua Chanzo cha elimu yake; kwa neno lingine tena daraja na hatima yake vililindwa. Yule Mkuu husema: Mchukulie mwanadamu kama chimbo la madini lililojaa vito vyenye thamani isiyokadirika. Elimu pekee, ndio inayoweza kulifanya lifichue hazina zake, na kuiwezesha jamii ya binadamu kunufaika kutoka humo. Ikiwa mtu yeyote atatafakari kile ambacho Maandiko matakatifu yaliyoshushwa kutoka mbingu ya mapenzi matakatifu ya Mungu, yamkiefunua, angetambua bila kusita kwamba kusudi lake ni kwamba watu wote wachukuliwe kama roho moja, ili kwamba muhuri wenye maneno haya 'Ufalme utakuwa wa Mungu' uweze kupigwa juu ya kila moyo, na mwanga wa baraka Takatifu, wa neema, na rehema uweze kufunika jamii nzima ya binadamu."**[22]

1. Mitume na Wajumbe wa Mungu wameteleshwa kwa kusudi gani? _______________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

2. Ni lipi kusudi la kimsingi la ufunuo Wao? _______________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

3. Neno "talasimu" lina maana gani? _____________________________________

_______________________________________________________________

4. Ni yapi madhara ya ukosefu wa elimu inayofaa? __________________________

_______________________________________________________________

5. Elimu inayofaa inaweza kusababisha nini? ______________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

6. Ni kipi Chanzo cha elimu yetu? ______________________________

7. Ni ipi hatma yetu? ______________________________

______________________________________________________________

8. Ni vipi baadhi ya vito ambavyo elimu huvifichua? ______________________________

______________________________________________________________

9. Tunatambua nini bila kusita pale tunapotaamuli juu ya Maandiko Matakatifu? _____

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 17

Bahá'u'lláh hutamka:

**"Wewe umeniuliza, zaidi, kuhusu hali ya roho baada ya kutengana kwake na mwili. Jua wewe, kwa ukweli, kwamba ikiwa roho ya mtu imetembea katika njia za Mungu, kwa hakika itarudi na kukusanyika kwenye utukufu wa Mpendwa. Kwa haki ya Mungu! Itafikia daraja ambalo hakuna kalamu inayoweza kulifafanua, wala ulimi kulielezea. Roho ambayo imebakia aminifu katika hoja ya Mungu, na kusimama imara bila kutetereka katika Njia Yake, baada ya kupaa kwake, itakuwa na ile nguvu kiasi kwamba maulimwengu yote aliyoyaumba Mwenyezi yaweza kunufaika kupitia kwake."**[23]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Ikiwa roho imetembea katika njia za Mungu, kwa hakika, ______________________________
   ______________________________________________________________ .

   b. Itafikia daraja ambalo ______________________________ .

   c. ________________ ambayo imebakia ________________ katika ______________ ya ____________ , na ______________________ bila kutetereka katika ____________ , baada ya ____________________ , itakuwa na ile ________________ kiasi kwamba malimwengu yote ambayo ______________________________ yaweza _________________ kupitia kwake.

## SEHEMA YA 18

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Imebarikiwa ile roho ambayo, wakati wa kuachana kwake na mwili, imetakasika kutokana na fikra za bure za watu wa ulimwengu. Roho kama hiyo huishi na hujongea kwa mujibu wa Mapenzi ya Muumba wake, na huingia katika paradiso ya juu kabisa. Wanawali wa Mbinguni, wakazi wa makasri bora kabisa, wataizunguka, na Mitume wa Mungu na wateule Wake watatafuta urafiki nayo. Pamoja nao roho hiyo itazungumza kwa uhuru, na itawasimulia yale ambayo ililazimika kuvumilia katika njia ya Mungu, Bwana wa maulimwengu yote."[24]**

**"Yeye anapaswa amsamehe mwenye dhambi, na kamwe asidharau hali yake ya chini, kwa kuwa hakuna ajuaye jinsi mwisho wake mwenyewe utakavyokuwa. Ni mara ngapi mwenye dhambi amefikia, wakati wa kifo, kwenye kiini cha imani, na akigugumiza funda la milele, amepaa hadi kwenye Umati wa juu! Na ni mara ngapi muumini mcha Mungu wakati wa kupaa kwa roho yake, amebadilika mno hata kutumbukia kwenye moto wa chini kabisa!"[25]**

1. Ni katika hali gani roho yetu inapaswa kuwa wakati wa kuachana na mwili?________

   ______________________________________________________________

2. Ni zipi baadhi ya fikra za bure? ______________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

3. Ni katika hali gani roho iliyotakasika kutokana na fikra za bure itaishi na kujongea baada ya kifo?_____________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

4. Nani watakuwa wenzi wa roho kama hiyo?__________________________

   ______________________________________________________________

5. Je, roho kama hiyo itaweza kuzungumza na Mitume wa Mungu na wateule Wake?

   ______________________________________________________________

6. Je, tunafahamu kabla jinsi gani na lini maisha yetu ya duniani yataisha? __________

   ______________________________________________________________

7. Tunaweza kufanya nini sasa ili kufikia maisha ya milele yaliyokusudiwa kwetu? ___

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 19

'Abdu'l-Bahá hueleza:

**"Kwa kuwa roho ya mwanadamu huishi milele baada ya kuvua umbo hili la kimwili, kama vitu vyote viishivyo, bila shaka ina uwezo wa kuendelea, na hivyo mtu anaweza kusali kwa ajili ya roho ya marehemu kuendelea, kusamehewa, au kufanywa kuwa mpokezi wa fadhili takatifu, rehema, na neema. Ndiyo maana, katika sala za Bahá'u'lláh, msamaha na ghofira ya Mungu huombwa kwa ajili ya wale waliopaa kwenye ulimwengu mwingine. Aidha, kama vile watu wanavyomhitaji Mungu katika ulimwengu huu, vivyo hivyo wanamhitaji katika uje ujao. Viumbe daima vipo katika uhitaji, na Mungu daima hawategemei kabisa, iwe katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao."[26]**

Kwa nini tunapaswa kusali kwa ajili ya roho za marehemu?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 20

'Abdu'l-Bahá huandika:

**"Wakati roho ya mtu inapopaa kutoka lundo hili la vumbi la mpito na kupanda kwenye ulimwengu wa Mungu, hapo tando zitapotea, na kanuni za Mungu zitaonekana, na vitu vyote vilivyokuwa havivyojulikana hapo awali, vitawekwa wazi, na kweli zilizofichika zitaeleweka.**

**"Fikiria jinsi kiumbe, akiwa katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, alikuwa kiziwi wa masikio na kipofu wa macho, na bubu wa ulimi; jinsi gani alivyokuwa amekosa utambuzi wowote. Lakini pindi, alipotoka katika ule ulimwengu wa giza, aliingia katika ulimwengu huu wa mwangaza, hapo macho yake yaliona, masikio yake**

**yakasikia, ulimi wake ukaongea. Vivyo hivyo, pindi atakapoharakia kutoka mahali hapa pa umauti kuingia katika Ufalme wa Mungu, hapo atazaliwa katika roho; ndipo macho ya utambuzi wake yatapofunguka, masikio ya roho yake yataposikia, na kweli zote ambazo hakuzijui hapo awali zitawekwa wazi na dhahiri."**[27]

1. Jaza nafasi zilizo wazi hapo chini.

   a. Wakati roho ya mtu inapouacha ulimwengu huu, hapo

      – tando ________________________ ,

      – na kanuni za Mungu_________________________ ,

      – na vitu vyote vilivyokuwa havivyojulikana hapo awali __________________ ,

      – na kweli zilizofichika _______________________ .

   b. Katika ulimwengu wa _________________ , sisi tulikuwa ______________ wa masikio, _____________ wa macho, na _________ wa ulimi.

   c. Tulipozaliwa katika ulimwengu huu, hapo macho yetu __________ , masikio yetu ____________ , na ulimi wetu ____________________ .

   d. Vivyo hivyo, pindi tutakapoharakia katika Ufalme wa Mungu, ___________ katika ________ .

   e. Hapo ndipo macho ya _____________ wetu ________________ , masikio ya __________ yetu ________________ , na ___________ zote ambazo hatukuzijua hapo awali ____________________ na _____________ .

2. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

   _____ Tunapokuwa katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, tunajua kuhusu ulimwengu huu.

   _____ Hali yetu baada ya kifo ni ukweli uliofichika kwetu katika maisha haya.

   _____ Peo, mpya kabisa, zitafunguka mbele ya macho yetu baada ya kifo.

   _____ Tunapofariki, tunarudi kwenye ulimwengu huu kuzaliwa tena.

## SEHEMU YA 21

Bahá'u'lláh hueleza:

**"Na sasa kuhusu swali lako kama roho za wanadamu huendelea kutambuana baada ya kutengana kwao na mwili. Fahamu kwamba roho za watu wa Bahá,**

**ambao wameingia na wameimarishwa ndani ya Safina Nyekundu, watashirikiana na kuzungumza kirafiki mmoja kwa mwingine, na watashirikiana kwa ukaribu sana katika maisha yao, matamanio yao, malengo na jitihada zao hata kuwa kama vile roho moja. Kwa hakika wao ni wale ambao wamejazwa vyema, ambao wana utambuzi makini, na ambao wamejazwa uelewa. Hivyo ndivyo ilivyoamriwa na Yeye Ambaye ndiye Mjua-Yote, Mwenye Hekima-Kabisa.**

**"Watu wa Bahá, ambao ni wakazi wa Safina ya Mungu, kila mmoja na kwa pamoja, wanatambua vyema hadhi na hali ya mwenzake, na wameunganika katika mafundo ya urafiki wa karibu sana na undugu. Hadhi kama hiyo, hata hivyo, sharti itegemee juu ya imani yao na mwenendo wao. Wao ambao ni wa ngazi na daraja moja wanatambua kikamilifu uwezo, tabia, mafanikio na ustahili wa kila mmoja wao. Wale ambao ni wa ngazi ya chini, walakini, hawawezi kufahamu kikamilifu daraja, au kukadiria ustahili wa wale walio katika safu ya juu yao. Kila mmoja atapokea fungu lake kutoka kwa Bwana wenu. Amebarikiwa yule ambaye amegeuzia uso wake kwa Mungu na kutembea kwa uthabiti katika upendo Wake, hadi roho yake itakapopaa kwendanda kwa Mungu, Bwana Mwenye Mamlaka juu ya vyote, Mwenye Nguvu-Kabisa, Msamehevu-daima, Mwenye Rehema-kabisa."[28]**

1. Je, katika ulimwengu ujao tutawatambua watu ambao tumewafahamu katika ulimwengu huu? ____________________

2. Je, ushirikiano kati ya roho utakuwa wa ukaribu jinsi gani katika ulimwengu ujao? ____________________

3. Je, utofauti na upekee miongoni mwa roho utategemea juu ya nini katika ulimwengu ujao? ____________________

4. Je, kuna yeyote atakayenyimwa neema ya Mungu? ____________________

## SEHEMU YA 22

Bahá'u'lláh hutusihi:

**"Enyi watumishi Wangu! Msihuzunike iwapo, katika siku hizi na kwenye uso huu wa dunia, mambo yaliyo kinyume na matakwa yenu yakiamriwa na kudhihirishwa na Mungu, kwa kuwa siku za furaha tele, za nderemo za mbinguni, kwa hakika zimewekwa akiba kwa ajili yenu. Malimwengu, matakatifu na yenye utukufu wa kiroho, yatafunuliwa machoni penu. Mmekusudiwa na Yeye, katika ulimwengu huu na ule ujao, kujitwalia sehemu ya manufaa yao, kushiriki katika furaha zao, na kujipatia sehemu ya neema yao ya kudumu. Kwa kila moja yao bila shaka mtayafika."[29]**

1. Amua ni yapi kati ya yafuatayo ni kweli:

_____ Tunapaswa tujazwe na huzuni pale mambo yasipoenda kama tutakavyo.

_____ Yote, yawe mema au mabaya, yameamriwa na Mungu.

_____ Siku za furaha tele zinatusubiri sote.

_____ Tuna hakika kuyaona malimwengu ambayo ni matakatifu na matukufu kiroho.

_____ Ni hatma yetu kujitwalia manufaa ya malimwengu ambayo ni matakatifu na matukufu kiroho, katika maisha haya na maisha yajayo.

2. Kwa nini hatupaswi kujawa na huzuni pale mambo yanapotokea kinyume na matakwa yetu? ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

3. Bahá'u'lláh anatuahidi nini katika kifungu hiki? ______________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

## SEHEMU YA 23

Katika kitengo hiki, mmetafakari juu ya maana ya maisha ya mwanadamu. Mmejifunza mengi kuhusu asili ya roho, kusudi la maisha katika ulimwengu huu, ulazima wa kukuza sifa za kiroho na ahadi tuliyopewa ya uzima wa milele, mtukufu na uliojawa na shangwe. Katika kitengo cha pili cha kitabu hiki, tuliongelea juu ya kusudi lenye pande mbili—kufuatilia ukuaji wetu wenyewe wa kiroho na wa kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Hapa kuna fursa ya kurejea kwenye dhana hiyo na kufikiria juu ya umuhimu wa kudhughulikia sura zote mbili za kusudi hili, kufuatana na umaizi ambao mmeupata juu ya maendeleo ya roho. Tafakari zenu zinaweza kunufaika kutokana na majadiliano juu ya mada za hapa chini katika kikundi chenu.

1. *Kukuza sifa za kiroho*
2. *Kutii sheria za Mungu*
3. *Kuchangia kwenye ustawi wa mbari ya wanadamu*
4. *Kusonga mbele kwenye njia ya huduma*

# MAREJELEO


1. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa 10 Novemba 1911, yaliyochapishwa katika *Hekima ya ‘Abdu’l-Bahá (Mazungumzo ya Paris): Hotuba Zilizotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, chapisho la 2016), na. 29.12–13, uk. 109.

2. Kutoka barua ya 1 Aprili 1946 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, iliyochapishwa katika *Lights of Guidance: A Bahá’í Reference* [Miangaza ya Uongozi: Faili la Marejeleo ya Kibahá’í] (New Delhi: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, chapisho la 2010), na. 1820, uk. 537. (toleo la Kiingereza)

3. Kutoka barua ya 28 Julai 2016 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

4. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Some Answered Questions* [Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa] (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’i, 2014, chapisho la 2016), na. 66.3, ku. 352–53. (toleo la Kiingereza)

5. Kama hapo juu, na. 38.5, uk. 220.

6. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá 9 Novemba 1911, yaliyochapishwa katika *Hekima ya ‘Abdu’l-Bahá (Mazungumzo ya Paris*), na. 28.16, uk. 104.

7. Kutoka baruaya 31 Decemba 1937 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, iliyochapishwa katika *Lights of Guidance* [Miangaza ya Uongozi], na. 680, uk. 204.

8. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, chapisho la 2017), LXXXII, aya. 8, uk.183. (toleo la Kiingereza)

9. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Some Answered Questions* [Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa], na. 61.1–2, uk. 334.

10. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, LXXX, aya. 2, uk. 174.

11. Kama hapo juu, LXXXI, aya. 1, uk. 176.

12. Kama hapo juu, CLXV, aya. 1–3, ku. 391–92.

13. Bahá’u’lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá’í wa Tanzania, toleo la 2017), Kiarabu na. 32, uk. 9.

14. Kutoka kwenye mazungumzo yaliyotolewa 6 Julai 1912, na kuchapishwa katika *The Promulgation of Universal Peace: Talks Delivered by ‘Abdu’l-Bahá during His Visit to the United States and Canada in 1912* [Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá wakati wa ziara Yake huko Marekani

na Canada mnamo 1912] (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), ku. 315–16. (tafsiri iliyoidhinishwa)

15. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, V, aya. 4, uk. 8.

16. Kama hapo juu, LXXXII, aya. 1, ku. 179–80.

17. Kama hapo juu, CLIII, aya. 6, ku. 370–71.

18. Kama hapo juu, XXVII, aya. 2, ku. 72–73.

19. Kama hapo juu, XXVII, aya. 3, uk. 73.

20. Kama hapo juu, XXI, aya. 1, ku. 54–55.

21. Kama hapo juu, LXXXI, aya. 1, uk. 177.

22. Kama hapo juu, CXXII, aya. 1, ku. 293–94.

23. Kama hapo juu, LXXXII, aya. 7, uk. 182.

24. Kama hapo juu, LXXXI, aya. 1, ku. 176–77.

25. Kama hapo juu, CXXV, aya. 3, ku. 300–1.

26. 'Abdu'l-Bahá, katika *Some Answered Questions* [Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa], na. 62.3, ku. 340–41.

27. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, chapisho la 2015), na. 149.3–4, ku. 246–47. (toleo la Kiingereza)

28. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LXXXVI, aya. 1–2, ku. 192–93.

29. Kama hapo juu, CLIII, aya. 9, uk. 373.